
SportPesa
TZS. 1,042,431,860
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Bunge** labaini matatizo ajira, fidia, wasiwasi ujenzi wa SGR

UKURASA 2



**MESSI, NEYMAR YAWAKUTA PSG**

UKURASA 22

Nipashe
Jumanne Machi 15, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580885
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Mshtakiwa adai Sabaya aliagiza afungwe pingu

• **Ni** katika kesi ya uhujumu uchumi, adai kupigwa makofi, kutishwa... *Endelea ukurasa 3*

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

**JESHI LAANZA UCHUNGUZI MOTO KIWANDA CHA GSM**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam limeanza uchunguzi wa chanzo cha moto...

**UKURASA WA 4**

**MAJALIWA AONYA MA-RC UKUSANYAJI WA MAPATO**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wakuu wa mikoa wahakikishe halmashauri zote nchini zinatumia...

**UKURASA WA 5**

**SERIKALI: HAKUNA SHIDA DENI LA TAIFA**

KATIBU Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, amesema Deni la Taifa ni himilivu na serikali ina...

## Nape ajivunia kanuni, ukuaji wa Sekta ya Habari

UKURASA 2



UKURASA 2

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba (kulia), akimjulia hali miongoni mwa majeruhi wa ajali ya basi la Kampuni ya Kilimanjaro, Salama Sanga, lililopinduka Senjele wilayani Mbozi, jana. **PICHA NA GRACE MWAKALINGA**



Kamanda Rashid Ngonyani

# Ajali ya basi ilivyoua wanne, kujeruhi 36

**MICHEZO** KIDUKU AJA NA 'HESHIMA KWA MAMA' UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Ajali ya basi ilivyoua wanne na kujeruhi 36

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WATU wanne wamefariki dunia papo hapo na wengine 36 kujeruhiwa katika ajali ya basi la Kilimanjaro lililotumbukia kwenye korongo wakati dereva akijaribu kulipita lori eneo la Senjele wilayani Mbozi mkoani Songwe.

Taarifa ya Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Rashid Ngonyani, jana ilibainisha kuwa ajali hiyo ilitokea majira ya saa moja asubuhi kwenye mteremko wa Senjele baada ya dereva wa basi la Kilimanjaro linalofanya safari zake kutoka mjini Tunduma kwenda Dar es Salaam, Mjahidi Waziri (39), kuwa kwenye mwendokasi akijaribu kulipita lori.

Ngonyani alisema wakati Waziri akijaribu kulipita lori hilo, alikutana na lori lingine na kuamua kulipeleka basi hilo kwenye korongo hali iliyosababisha maafa. "Chanzo cha ajali mwendokasi wa dereva wa basi ambapo alikuwa anayafukuzia mabasi mengine mbele yake na yeye bila kuchukua tahadhari aliamua kuyapita malori mengine na kisha kukutana na gari lingine mbele ndipo akaamua kulipeleka basi lake korongoni," alisema Kamanda Ngonyani.

Kamanda Ngonyani alisema baada ya kutokea kwa ajali hiyo, dereva Waziri aliamua kujisalimisha polisi na hadi sasa anashikiliwa na wanatarajia kumfikisha mahakamani pamoja na kunyang'anywa leseni yake ya udereva.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, alisema majeruhi 36 wa ajali hiyo wanaendelea kupatiwa matibabu na afya zao zinaendelea kuimarika.

Alisema basi hilo lilibeba abiria 40 kati yao wanne ambao wote ni wanaume walipoteza maisha papo hapo huku wengine 36 wakiwamo saba walikimbizwa katika Hospitali Teule ya Ifisi iliyoko wilayani Mbeya na 29 wakipatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Songwe.

Alisema kati ya majeruhi hao, wawili wamepewa rufani kwenda kutibiwa kwenye Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH) kwa ajili ya matibabu zaidi.

Akiwa Hospitali ya Ifisi, Mgumba aliwapa pole majeruhi wote na kuwahakikishia kupatiwa matibabu na kurejea kwenye majukumu yao ya kulijenga taifa.

Alikemea tabia ya madereva wa mabasi kuendesha magari yao kwa mwendokasi bila kuchukua tahadhari na kwamba serikali itaendelea kuwachukulia hatua wote wanaosababisha vifo na majeruhi.

Baadhi ya majeruhi wa ajali hiyo, Claud Edward, mkazi wa jijini Dar es Salaam, aliyepata majeraha maeneo ya kichwani na mkononi, alisema dereva wa basi la Kilimanjaro alikuwa anaendesha gari hilo kwa mwendokasi kufukuzia mabasi mengine yaliyokuwa mbele yake.

Alisema baada ya kukutana uso kwa uso na lori dereva alichukua uamuzi wa kulipeleka gari kwenye korongo ili kulipisha lori lipite na kusababisha madhara hayo.

Yusuph Ramadhan ambaye ni mkazi wa jijini Dar es Salaam, alisema amepata majeraha maeneo ya mkononi na kwenye mbavu huku akiomba serikali kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa madereva ambao wanaendesha kwa mwendokasi.



Mkurugenzi wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET), Dk. Geofrey Oleke (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu udahili wa wanafunzi katika mkupuo utakaoanza mwezi huu kwa vyuo vyote isipokuwa vinavyotoa mafunzo ya afya na sayansi shirikishi, kulia ni Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa baraza hilo, Hawa Mwambulukuta. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Nape ajivunia marekebisho kanuni na ukuaji kidigitali

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imefanya marekebisho ya kanuni za maudhui ya mtandaoni za mwaka 2020, ikiwamo kupunguzwa ada ya maombi ya leseni kutoka Sh. 100,000 hadi Sh. 50,000 na ada ya mwaka kutoka Shilingi milioni moja hadi Sh. 500,000.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akieleza mafanikio ya mwaka mmoja ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Nnauye alisema kanuni hizo zimefanyiwa marekebisho ili kuboresha matumizi ya mtandao na kukuza fursa, ajira na vipaji kwa vijana wa kitanzania.

Alisema serikali vilevile imefanya marekebisho ya kuondoa leseni kwa watoa maudhui mbalimbali ikiwamo mapishi, michezo, usanii kama vile mziki na filamu.

"Kwa marekebisho haya, habari na matukio ya sasa yaani 'news and current affairs' ambayo hutolewa pia na vyombo vya habari vya kawaida ndiyo zitakazokatiwa leseni na pia kutakuwa na leseni kwa wakusanya habari mbalimbali wenye lengo la kuzitoa kwa watoa maudhui ya habari mtandaoni," alisema Nape na kuongeza:

"Pia serikali imeondoa hitaji la leseni ya Simulcasting. Hii ni kwa watoa huduma wa maudhui wanaotoa maudhui kwa njia ya redio ama televisheni, wanapotaka kwa wakati huohuo kutoa matangazo hayo kwa njia ya mtandao hawatahitaji leseni nyingine."

Nape alisema pia serikali imeondoa zuio la matangazo ya michezo ya kubahatisha inayofanyika katika mtandao yataendelea kusimamiwa na sheria ya nchi ya kubahatisha na kueleza kwamba serikali iliona hakuna haja ya kuwa na zuio katika kanuni hizo.

Aidha, alisema serikali pia imefanya marekebisho katika kanuni za utangazaji katika redio na televisheni ili kuvutia uwekezaji.

Akifafanua maeneo yaliyofanyiwa marekebisho, Nape aliyataja kuwa ni kuainisha wigo wa utoaji huduma kwa leseni za utangazaji kwa leseni za kiwilaya, kwamba leseni moja itatumika hadi maeneo matatu ya mkoa.

Alitaja eneo lingine ni kuondoa zuio la wageni kutembelea studio na pia kutoa maudhui katika studio bila kuambatana na ofisa wa serikali.

Kadhalika, Nape alisema kipindi cha mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani kumekuwa na uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya mawasiliano.

"Kuanzia Machi, 2021 hadi Februari 2022 laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka milioni 51.2 hadi milioni 55.39. Idadi ya akaunti za pesa kupitia simu za mkononi imeongezeka kutoka milioni 27.32 hadi milioni 32.72, watumiaji wa huduma za mtandao imeongezeka kutoka milioni 28 hadi milioni 30."

Alisema serikali baada ya kuimarisha mahusiano na vyombo vya fedha duniani, imewezesha kutiwa saini na kuidhinishwa kwa Mradi wa Tanzania ya Kidijitali wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 50 ambao utatekelezwa kwa mkopo wa Benki ya Dunia.

Kadhalika, mkataba huo ulitiwa saini Agosti mwaka jana kisha kuanza kutekelezwa Novemba mwaka huo huo.

## Bunge labaini matatizo SGR

**Na Richard Makore,** MWANZA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu imebaini matatizo katika ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha tano kati ya Fela mkoani Mwanza na Isaka mkoani Shinyanga.

Miongoni mwa matatizo yaliyobainika ni kasi ndogo ya ujenzi, kutoonekana mitambo ya ujenzi eneo la mradi, kutolipwa fidia ya mashamba ya wananchi pamoja na vijana wazalendo kubaguliwa katika ajira za mradi huo.

Wajumbe wa kamati hiyo walibainisha dosari hizo jana katika ziara waliyofanya ya kutembelea mradi huo kati ya Mwanza na Isaka.

Mjumbe wa kamati hiyo na Mbunge wa Kyela, Ally Msagila, akizungumza katika kikao cha majumuisho ya ziara hiyo, alisema mtu akiangalia kwa macho anaona kazi hairidhishi.

Alisema mradi huo ambao utagharimu Sh. trilioni 3.6 unahitaji kusimamiwa kwa karibu ili ulete tija.

Mbunge wa Sumbawanga, Aeshi Hilary, alisema wabunge hawajaona vifaa vinavyotumika katika ujenzi eneo la mradi na kwamba hali hiyo inaleta wasiwasi.

Mbunge wa Viti Maalumu, Sophia Mwakagenda, akizungumza katika ziara hiyo, alisema mradi huo unasuasua na hadi sasa umefika asilimia nne tu tangu ulipoanza Mei mwaka jana.

Alisema malalamiko ya wananchi katika mradi huo yamekuwa mengi ikiwamo kukosa ajira pamoja na kutolipwa fidia ya mashamba yao eneo la Fela ili kupisha mradi huo Sh. milioni 800.

Akijibu hoja za wabunge hao, Meneja wa Mradi huo kutoka Shirika la Reli (TRC), Machibya Masanja, alikiri ujenzi huo kufikia asilimia 4.46 huku tuta linalobeba reli likiwa limefikia asilimia 10.

Meneja huyo alisema malipo waliyotoa kwa mkandarasi ni asililimia 15, sawa na Sh. bilioni 376.4.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, akijibu baadhi ya hoja za wabunge, alisema serikali imetenga Sh. trilioni 14.5 kukamilisha ujenzi wa SGR kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza.

Alibainisha kuwa mpaka sasa serikali imetumia Sh. trilioni 7.7 na hakuna mkandarasi anayedai huku akiahidi serikali itaangalia njia nzuri ya kuwapatia ajira vijana wazalendo ili wanufaike na mradi huo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Seleman Kakoso, aliitaka TRC kusimamia mradi huo kwa uzalendo ili wananchi wanufaike nao.

Alisema mradi huo umetoa kiasi kidogo cha huduma za jamii ambacho ni Sh. bilioni 1.8 wakati fedha za kujenga mradi huo zinafikia Sh. trilioni 3.6.

Jana asubuhi kundi kubwa la wananchi katika eneo la Fela unakojengwa mradi huo, lilisimamisha msafara wa kamati hiyo, wakipaza kilio chao kuhusu kunyimwa ajira katika mradi huo na wengine kutolipwa fidia ya maeneo yao.

HABARI KITAIFA

# Mshtakiwa: Sabaya aliagiza nifungwe pingu na nipigwe

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHAHIDI wa tano wa utetezi, Watson Mwahomange (27), amedai mahakamani kwamba aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Lengai, Ole Sabaya (Pichani), aliagiza apigwe vibao vya masikioni, kufungwa pingu na kupelekwa katika karakana ya mfanyabiashara Francis Mroso iliyoko Mbauda jijini Arusha.

Shahidi huyo ambaye ni mshtakiwa wa tatu katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili Sabaya na wenzake sita, alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Dk. Patricia Kisinda.

Akijitetea mahakamani huko, shahidi huyo alidai ni mkazi wa Azimio Sakina jijini Arusha na anajihusisha na upigaji picha, akidai anafahamu anakabiliwa na mashtaka ya kutakatisha fedha na kuunda genge la uhalifu.

Mwahomange alidai kuwa Januari 20, 2021, akiwa nyumbani kwao Sakina, majira ya asubuhi, alipigiwa simu ya Sabaya kwa namba mpya.

Alidai kuwa baada ya kupokea simu hiyo, Sabaya alimsalimia na akamuuliza kuhusu alikokuwa na alimjibu kwa alikuwa nyumbani.

"Sabaya aliniambia mwenye namba ya simu hiyo kuwa yupo njiani anakuja Arusha, hivyo alinitaka kujiandaa kwenda kukutana naye na baada ya dakika 15 huyo mtu niliyeambiwa nitakutana naye, alinipigia na kunieleza amepewa namba na Mkuu wa Wilaya ya Hai, hivyo aliniuliza wapi pa kukutana.

"Nilimwambia tukutane eneo la Florida, baada ya dakika 15 alipiga tena akinitaka kutoka nyumbani kwa kuwa alikuwa ameshafika Tengeru," shahidi alidai.

Alidai kuwa alipofika Florida, alitoa simu yake na kumpigia mhusika lakini simu yake ilikuwa inafanya mawasiliano na baadaye alimpigia akimtaka kwenda Mbauda kwa kuwa alishaondoka eneo walikokuwa wamepanga kukutana awali.

Shahidi huyo alidai kwamba alipofika Mbauda, alimkuta kwenye gari nyeusi aina ya Benzi, akashusha kioo na akaingia kwenye gari kisha akapewa pampu na Sabaya na akatakiwa kwenda kuisimamia ili itengenezwe.

"Nikamuuliza 'nikatengeneze wapi?' Yule mtu alinielekeza sehemu ya kwenda kutengeneza na kuhusu malipo aliniambia ikishatengenezwa niwapatie taarifa.

"Yule mtu aliniambia anakwenda Makuyuni, hivyo nilishuka kwenye gari nikiwa nimebeba boksi lenye pampu na nikavuka barabara hadi kwenye karakana hiyo na nilipokewa na fundi wa hapo.

"Niliongozana na fundi huyo tukaingia kwenye chumba kimoja ambacho kimegawanywa mara mbili, kimoja kilikuwa na mashine na kingine ni ofisi, tuliingia humo.

"Tulipofika ndani tulimkuta karani mzee ambaye alikuja hapa mahakamani kama shahidi wa nne wa mashtaka na alichukua pampu na kumweleza ilikuwa na tatizo la kutokuvuta na aliichukua na kuingiza kwenye mashine kuipima na baada ya hapo alichukua kitabu cha kusajili majina ya wateja na alinitaka kujisajili hapo.

"Nilichukua kitabu na kujisajili na baada ya hapo alipeleka pampu kwenye mashine na baada ya dakika 10 kupita, ilirudishwa na Mroso ambaye ni shahidi wa 10 wa mashtaka na alikuwa na karatasi ya gharama ya kuichunguza Sh. 45,000 na vitu vilivyokufa kwenye pampu," alidai.

Shahidi huyo alidai kwamba alipopewa karatasi hiyo, Mroso aliondoka na baada ya muda Sabaya alimpigia simu kwa kutumia simu ya Silvester akiuliza kwa nini anapigiwa simu hapokei.

"Alikata simu kwa kuwa anafahamu Sabaya ni mtata, nilimwomba yule mzee kuipiga picha ile karatasi ili kumtumia gharama ya matengenezo ya pampu.

"Nikiwa nipo sehemu napata chai nilitumiwa Sh.105,000 kwa namba ya Haloteli na nilikwenda kuitoa na kurejea pale gereji kusubiri pampu. Nilikaa kwa zaidi ya saa tatu baadaye niliondoka na nilichukua namba ya fundi mmoja ili anipigie simu pampu itakapokamilika kutengenezwa na nilielekea mjini," alidai.

Shahidi huyo alidai mahakamani kwamba baada ya saa moja kupita, alipigiwa simu kujulishwa kuwa pampu ilikuwa tayari na kwamba wakati akilipa fedha za matengenezo, alijaribu kutoa risiti ya kielektroniki lakini mashine ilikataa.



"Yule mzee aliniambia mtandao unasumbua, aliniomba kuniandikia pembeni nilimwambia aliyeniagiza ni mtata, alinieleza endapo atanisumbua nirudi kwa kuwa mtandao utakuwa umerejea na baada ya hapo niliwasiliana na yule aliyenipatia pampu hiyo kutengenezwa.

"Aliniambia yupo njiani eneo la Kisongo, alinitaka kumsubiria katika kituo cha mafuta cha Meru na baada ya dakika tano alifika na niliingiza pampu hiyo nyuma ya buti ya gari, na baada ya hapo alinipatia lifti hadi Triple A aliponishusha na mimi nilielekea nyumbani," alidai.

Pia alidai kwamba Januari 22, 2021 majira ya saa saba mchana, akiwa mjini Arusha, alipigiwa simu na Silvester akimweleza kwamba Sabaya anamwita katika hoteli ya Point Zone.

"Nilijaribu kumkatalia kwa kumwambia kuwa nipo mbali na sina hata hela, baada ya nusu saa nilichukua pikipiki kuelekea Point Zone wakati tunakaribia kufika nilikutana na gari tatu ikiwamo gari ya serikali STL V8 nyeupe, Prado na VX Masai zilikuwa zinaingia kwenye hoteli hiyo.

"Alishuka Sabaya na vijana wengine wakanizunguka huku akiniambia mimi ni nani ananiita muda wote halafu sijafika na kulikuwa na kijana mmoja anaitwa Shukuru na alitoa ile karatasi ya malipo ya pampu na kumkabidhi Sabaya.

"Sabaya alikuwa akiongea kwa hasira sana, akiniambia kwa nini kila akinituma ninaongeza bei ya kitu na niljmjibu kuwa sijaongeza bei, akasema ninamfanya yeye ni mtoto, hivyo alimwagiza Shukuru 'kunitoa loku' (kupiga vibao vya masikio) huku akisema akikuta nimeongeza hata shilingi 100 ataniweka rumande," alidai.

Shahidi huyo alidai kuwa baada ya sakata hilo, alimwagiza Shukuru na kijana mwingine kumkamata na kumfunga pingu ili asitoroke na walimwigiza katika gari ya VX Masai.

"Yale magari yalielekea hadi Kwa Mroso kwenye karakana yake bila ya mimi kuwaelekeza na watu walishuka kwenye magari, lile gari la STL lilikuwa likiendeshwa na dereva wa serikali na zilipaki uelekeo wa kuondoka kwenye lango la kuingilia na kutokea na mimi nilikuwa bado nipo ndani ya gari.

"Baada ya muda kupita, alikuja mlinzi wa Sabaya akielekeza kufunguliwa pingu na walinibebesha boksi la pampu na tuliingia hadi kwenye ofisi na tulimkuta Sabaya amesimama akiwa na karani pamoja na Mroso.

"Waliponifikisha pale Sabaya aliniuliza kwa nini alinituma, lakini sikupatiwa risiti, aliagiza nitolewe eneo lile huku akiwa amebaki na karatasi na boksi. Walinirudisha kwenye gari nikiwa sijafungwa pingu.

"Yule kijana aliyekuwa ananilinda na kunifunga pingu aliniambia kwamba nina bahati kwa kuwa nilikuwa nikalale rumande. Wakati akizungumza hivyo, machozi yalikuwa yananitoka kwa kuwa Januari 20, 2021 nilitumwa kwenda kutengeneza pampu na sikulipwa kitu chochote, wamenifunga pingu na kutolewa loku.

"Kijana yule aliitwa na Sabaya kule ndani kwenye ofisi ya Mroso, hivyo nilibaki mwenyewe kwenye gari. Nilishuka nikachukua toyo (pikipiki) na kutoroka na kwenda nyumbani na yaliyoendelea baada ya hapo sifahamu kwa kuwa sikuwapo.

"Ni kweli kwamba Mroso alieleza mahakamani kwamba ananifahamu kama kijana wa Sabaya kwa kuwa nilipeleka pampu kutengenezwa, pia alieleza kwamba hakuwahi kunipa rushwa wala sikuwapo benki ya CRDB Kwa Murombo wakati akitoa fedha," alidai.

Kuhusu kuunda genge la uhalifu katika Hoteli ya Point Zone, shahidi alidai hafahamu kwa kuwa wakati akielekea eneo hilo, alikuta magari, moja likiwa limembeba Sabaya.

"Siyo kweli kwamba nilifungwa pingu ili kutengeneza mbinu ya kumtisha Mroso ili atoe Sh. milioni 90 na kuanzia shahidi wa kwanza hadi 12 hakuna shahidi aliyesema amenipatisha rushwa au kuniona wakati wa makabidhiano.

"Kwa mujibu wa hati ya mashtaka inaonyesha machakato wa rushwa ulianzia Kwa Murombo na Mroso alipokuja hapa mahakamani alieleza kuwa hakuwahi kunipa rushwa, pia baada ya kutoka Kwa Murombo nilikwenda nyumbani, hivyo Tulia Lodge sikwenda kabisa wala kupewa mgao wowote," alidai.

Shahidi huyo alikiri kwamba alikamatiwa jijini Dar es Salaam Juni 24, 2021 na shahidi wa 11 wa Jamhuri Hemed Shaban, Ofisa Uchunguzi wa TAKUKURU.

### KORTI YAKATAA OMBI

Katika hatua nyingine, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha imetupilia mbali ombi la shahidi wa tatu wa utetezi katika kesi hiyo, Watson Mwahomange, la kumpatia simu yake ili aitumie wakati akijitetea kizimbani.

Shahidi huyo ambaye ni mshtakiwa wa tatu katika kesi hiyo, alitoa maombi hayo mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi, Dk. Patricia Kisinda.

Akitoa uamuzi huo jana, Hakimu Kisinda alisema kutokana na ombi la shahidi huyo la kupatiwa simu hiyo, mahakama imeona halipo kisheria.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

# Jeshi laanza uchunguzi moto kiwanda cha GSM

**Na Jenifer Gilla**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es Salaam limeanza uchunguzi wa chanzo cha moto kwenye kiwanda cha magodoro cha kampuni ya GSM kilichoko Mikocheni.

Limesema timu ya wataalamu wake imeenda eneo la tukio na kwa kushirikiana na wamiliki, wanachunguza kilichosababisha kuzuka kwa moto huo ulioteketeza mali za mamilioni ya shilingi.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Jeshi la Zimamoto Kinondoni, Christina Sungwa, alisema walianza uchunguzi huo jana na wanategemea kumaliza kazi ndani ya wiki moja.

"Timu ya uchunguzi hivi sasa ipo site (eneo la tukio) kwa hatua za awali za uchunguzi. Tunafanya tathmini kujua chanzo cha moto pamoja na hasara iliyopatikana. Hadi mwishoni mwa wiki hii tutakuwa na majibu," alisema.

Akizungumza na Nipashe juzi, mmoja wa wasimamizi wa kampuni hiyo, Salah Mohamed, alisema alipata taarifa za kuungua moto kwa jengo hilo majira ya saa 12 asubuhi.

"Nilipigiwa simu na kaka yangu akiniambia 'bwana GSM foam Mwenge pale panawaka moto, hebu angalia nini tunaweza kufanya'. Kwa hiyo nikafika harasa na tukaanza kufanya mawasiliano. Ninashukuru Jeshi la Polisi walifika mapema tu," alisema Salah.

Alisema baada ya taarifa hiyo, walifanya mawasiliano sehemu mbalimbali walifanikiwa kupata magari ya zimamoto na kuzima moto huo lakini mali katika ghala hilo zilikuwa zimeshateketea.

"Kwa kweli mpaka sasa hatujui ni kiasi gani cha mali kimeteketea, ninachoweza kusema hasara ni kubwa sana, kama unavyoona hakuna kilichosalia," alifafanua.

Kiwanda hicho kiliungua moto juzi alfajiri na kuteketeza mali zote zilizokuwamo.



Meneja wa kiwanda cha kutengeneza na kuunganisha magari cha GFA Vehicle Assemblers, Ezra Mereng (wapili kulia), akimweleza Waziri wa Viwanda Biashara na Uwekezaji, Dk. Ashatu Kijaji, jinsi wanavyofanya kazi wakati Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilipotembelea kiwanda hicho kilichoko Kibaha mkoani Pwani jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vyombo vya usafiri 2,958 vyanaswa ukiukwaji wa sheria

**Na Jenifer Gilla**

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, limekamata vyombo vya usafiri 2,958 kutokana na wamiliki na madereva wake kwenda kinyume na matakwa ya Sheria ya Usalama Barabarani ya matumizi holela ya ving'ora, vimulimuli na taa za kubadili rangi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, SACP Wilbroad Mutafungwa, alisema walikamata magari hayo katika doria na msako barabara kuu za mikoa yote Tanzania Bara.

"Magari yaliyokamatwa yakiwa na vimulimuli na ving'ora visivyo rasmi ni 1,527, hii inajumuisha magari madogo na malori. Idadi ya pikipiki na bajaji ni 1,358 na idadi ya magari ya watu binafsi na ya serikali yaliyokamatwa yakitumia namba bandia ni 73," alifafanua.

Alisema doria hiyo imefanyika kufuatia tangazo walililotoa Februari 10, mwaka huu, la kuwataka wananchi kuacha matumizi holela ya vifaa hivyo kinyume na Sheria ya Usalama Barabarani ya mwaka 1973 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Alisema matumizi hayo yamekuwa yakisababisha usumbufu kwa watumiaji wengine wa barabara pamoja na kutengeneza fursa kwa wahalifu kutumia njia hiyo kukimbia baada ya kufanya uhalifu.

"Msako na doria bado inaendelea katika mikoa yote, tunazidi kuwakumbusha wamiliki na madereva wa magari kuondoa namba bandia, vimulimuli na ving'ora kwenye magari yao ili kuepuka kukamatwa barabarani na kuchukua hatua za kisheria," alisema.

Kamanda Mutafungwa alifafanua kuwa magari yanayopaswa kutumia vifaa hivyo kwa dharura ni ya kubeba wagonjwa (ambulance), zimamoto, vyombo vya ulinzi na usalama na yaliyopatiwa kibali na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na kutangazwa na Gazeti la Serikali.

Kadhalika, alisema mtu yeyote anayetaka kutumia vifaa hivyo vya dharura anapaswa kuomba kibali kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi au kwa Jeshi la Polisi na iwapo atakubaliwa atasindikizwa kwa kutumia ving'ora na sio vinginevyo.

# Majaliwa aonya ma-RC ukusanyaji wa mapato

**Na Mwandishi Maalumu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka wakuu wa mikoa wahakikishe halmashauri zote nchini zinatumia vizuri mashine na mifumo iliyowekwa katika ukusanyaji wa mapato.

Vilevile, amewataka wakuu wa mikoa wasimamie uadilifu kwenye ukusanyaji wa mapato, akisisitiza wajiridhishe kama kinachokusanywa na kinachopelekwa ni halisi.

"Lazima suala hili lisimamiwe kwa nguvu zote. Moja ya ajenda kubwa ni mapato, ukusanyaji wa mapato iwe ajenda namba moja katika ratiba zenu za utendaji kazi za kila siku," Majaliwa aliagiza alipozungumza na viongozi hao katika kikao alichokiendesha kwa njia ya video akiwa ofisini kwake Mlimwa jijini Dodoma jana.

Alisema iwapo hawatasimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato, bajeti zao hazitoongezeka na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Majaliwa alisema viongozi hao wanatakiwa wajiridhishe kama watendaji wa halmashauri wanamudu kufikia vyanzo vyote vya mapato, kuviratibu na kutumia mifumo sahihi ya ukusanyaji.

"Msiwaachie TAMISEMI pekee kusimamia ukusanyaji wa mapato, twende tukasimamie kwenye halmashauri zetu ili kuhakikisha makusanyo hayo yanaongezeka kila siku," aliagiza.

Waziri Mkuu aliwataka watendaji hao wahakikishe wanasimamia vizuri miradi mbalimbali inayotekelezwa katika maeneo yao na lazima ilingane na kiwango cha fedha kilichotolewa.

Pia aliwataka Watanzania wajivunie mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka mmoja wa serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

## Rais Samia apongezwa kwa kusimamia demokrasia

**Na Sabato Kasika**

RAIS Samia Suluhu Hassan amepongezwa kwa kusimamia haraka utawala bora na kuimarisha demokrasia nchini ndani ya kipindi cha mwaka mmoja tangu amekaa madarakani.

Pongezi hizo zilitolewa juzi na Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, alipokuwa akitoa tathmini ya taasisi hiyo kuelekea mwaka mmoja wa Rais Samia.

Akizungumza na waandishi wa habari, alisema katika kipindi cha mwaka mmoja Rais Samia amefanya mambo mengi makubwa hasa ya utawala ikiwamo kuagiza watu walioko mahabusu bila ushahidi kuachiwa huru.

"CEGODETA tunahusika na utawala bora, na tumeona mengi ambayo Rais amefanya ikiwamo kukaa na wapinzani na kuzungumza nao, lakini kuhakikisha mtu haonewi katika nchi hii," alisema Ngawaiya.

Aliongeza kuwa, Rais ameelekeza TAKUKURU kufuta kesi mbalimbali ambazo ushahidi wake ulikuwa haueleweki, na kwamba bado anaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha demokrasia na utawala bora.

"Rais pia amekuwa akikutana na watu wa makundi mbalimbali wakiwamo viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini ili kupata mawazo na ushauri, kutokana na kwamba kwa kuwa nchi inajengwa na wote, nasi tunashauri aendelee na utaratibu huo, kwani huo ni sehemu ya utawala bora," alisema.

Alisema mbali na hayo, Rais pia ameondoa mfumo dume, katika uongozi, kwa kuwa anatambua suala la uongozi ni kuwatumikia wananchi kwa manufaa ya taifa na kwamba awe mwanaume au mwanamke kwa kuwa wote wako sawa.

Alisema, CEGODETA ilijua tangu awali kuwa Rais Samia ana nafasi kubwa ya kufanya vizuri, kwa madai kwamba, alikuwa katika serikali iliyopita, aliona mengi na anajua ni wapi penye kasoro arekebishe na kuendeleza mazuri yote.

"Rais ameweza kuchambua, mambo yenye kasoro na kuyasahihisha sasa nchi inaneemeka, mahusiano ya kimataifa yameimarika, kwani miaka nyuma ni kama tulitaka kutengwa na mataifa mengine," alisema.

Alisema, Rais ameimarisha huduma za jamii ikiwamo afya kwa kuhakikisha Watanzania wanapata elimu kutoka kwa wataalamu wa afya ili kukabiliana na ugonjwa wa UVIKO-19 ambao ni janga la dunia.

Alisema hata kwenye elimu, ametumia vizuri fedha za UVIKO-19 kwa kujenga madarasa mengi na kununua madawati ya kutosha, na kwamba hatua hiyo imesaidia mwaka huu wasiwapo wanafunzi waliochaguliwa kidato cha kwanza walionza masomo kwa awamu.



Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya (katikati), akielezea tathmini ya taasisi hiyo ya mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan madarakani, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Katibu wa taasisi hiyo, Hamad Tao na Mjumbe wa Bodi ya CEGODETA, Erasto **Tumbo. PICHA: SABATO KASIKA**

# Serikali yasisitiza hakuna shida katika Deni la Taifa

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

KATIBU Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, amesema Deni la Taifa ni himilivu na serikali ina sifa ya kukopesheka, hivyo hakuna sababu Watanzania kuwa na wasiwasi.

Vilevile, amesema ili kujiimarisha vizuri kiuchumi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) walikubaliana kujiwekea utaratibu wa kuweka akiba ya fedha za kigeni isiyopungua miezi minne, zinazokidhi kuagiza bidhaa toka nje.

Tutuba alitoa kauli hiyo jana jijini Arusha alipofungua semina ya siku tatu ya wahariri wa vyombo vya habari iliyoandaliwa na Wizaya ya Fedha na Mipango.

Alisema kuwa kutokana na sifa ya kukopesheka, serikali inaendelea kutunza heshima hiyo ili iendelee kuaminika.

Tutuba alisema mikopo ya serikali inatoka kwa awamu tofauti na kila muda wa kurejesha deni unapofika, serikali imekuwa ikirejesha kwa wakati mkopo pamoja na riba kulingana na matakwa ya mkataba.

"Hapa kwenye Deni la Taifa nimeona niwatoe wasiwasi Watanzania kwa sababu serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imekuwa ikilipa Deni la Taifa kwa wakati kulingana na matakwa ya mkataba wa fedha zilizokopwa," alisema. Kuhusu akiba za fedha za kigeni walizojiwekea kwenye nchi za EAC, alisema Tanzania ina akiba ya zaidi ya miezi sita kwa ajili ya kuagiza bidhaa toka nje ya nchi kwa kipindi hicho.

"Tulijiwekea utaratibu huu wa kuweka akiba ya fedha za kigeni ili tuwe na uhakika wa kuwa na fedha za kutuwezesha kuagiza bidhaa toka nje," alisisitiza.

Kuhusu mfumuko wa bei, Katibu Mkuu alibainisha kuwa hadi kufikia Februari mwaka huu, ulikuwa umepungua hadi asilimia 3.7 toka zaidi ya asilimia nne Januari mwaka huu.

"Shilingi yetu inaendelea kuimarika ambapo kwa sasa mfumuko wa bei wa bidhaa mbalimbali nchini upo chini ya asilimia tano huku uchumi ukiendelea kuimarika," alisema. Tutuba alisema katika kusimamia miradi ya maendeleo, serikali imetumia zaidi ya Sh. trilioni 8.4 hadi kufikia Februari mwaka huu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati yake, Sh. trilioni 6.2 ni fedha za ndani na Sh. trilioni 2.2 ni fedha za nje.

Alisema kuwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo, serikali ilianzisha mfumo wa utumiaji wa mafundi jamii (Force Account) ili kupunguza gharama za kutekeleza miradi katika maeneo mbalimbali nchini. "Mfumo huu unapunguza gharama za ujenzi wa miradi ambapo taasisi na mashirika ya serikali yanapewa fedha za kutekeleza miradi katika maeneo yao, wananunua vifaa vyote na kuwatumia mafundi wa kawaida kujenga miradi hiyo na imetekelezeka kwa ufanisi mkubwa," alisema.

Katibu Mkuu alisema mfumo huo unakuwa na kamati ya usimamizi, ununuzi wa vifaa na mapokezi, lengo kubwa kuweka kamati hizo likiwa ni kuzuia mgongano wa maslahi.

Kwa mujibu wa Tutuba, serikali inaendelea kutekeleza miradi mingi midogo na mikubwa, ikiwamo ya kimkakati, kwa kutoa fedha kwa wakati ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati.

# Operesheni wahamiaji haramu yazinduliwa

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amezindua operesheni maalumu ya kudhibiti wahamiaji haramu, akiwaonya maofisa wa Jeshi la Uhamiaji kutojihusisha na rushwa katika operesheni hiyo.

Uzinduzi huo ulifanyika jana mjini Kibaha na operesheni hiyo itatekelezwa katika maeneo mbalimbali ambayo yamekuwa yakitumika kama njia za wahamiaji haramu kuingilia kwenye mkoa huo.

Kunenge alisema hatamvumilia ofisa atakayebainika kujihusisha na vitendo vya rushwa wakati operesheni hiyo ikitekelezwa, akisisitiza hatua za kisheria dhidi yake zitachukuliwa.

Mkuu wa Mkoa alisema wahamiaji haramu ambao wamekuwa wakiingia kinyume cha utaratibu, baadhi yao wanadaiwa kukijihusisha na vitendo vya uhalifu na hivyo kuhatarisha usalama wa wananchi kwenye maeneo husika.

Kunenge alisema kufanyika kwa operesheni hiyo kutasaidia kupunguza vitendo hivyo na kuufanya mkoa uendelee kuwa salama.

Alitumia nafasi hiyo kuwaomba wamiliki wa viwanda katika mkoa huo kutoa ushirikiano kwa maofisa wa Jeshi la Uhamiaji watakapotembelea maeneo yao.

"Niwaombe wakuu wa mikoa wenzangu kutoa ushirikiano katika operesheni hii maana wapo wanaopita mikoa ya jirani wanakamatiwa Pwani. Ni wazi wapo watu wanawasaidia njia za kupita. Katika hili tukishirikiana kwa pamoja, tutakomesha hii hali," alisema.

Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Pwani, Omari Hassan, alisema operesheni hiyo itafanyika kwa siku 10 kuanzia Machi 14 hadi Machi 23, mwaka huu, huku shabaha kubwa ikiwa ni kudhibiti wahamiaji haramu.

Alisema Pwani ina fursa nyingi za kiuchumi ikiwamo viwanda vingi vilivyoko na vinavyoendelea kujengwa na miongoni mwa wageni wanaoingia na vibali halali kuja kufanya kazi, vikiisha wanabadilika na kuwa haramu.

Hassan alisema lengo lao ni kupambana na hali hiyo ya uwapo wa wahamiaji haramu, akiwaomba wakazi wa Mkoa wa Pwani kusaidia kwa kutoa taarifa kwenye vyombo husika pindi watakapoona kuna wahamiaji haramu katika maeneo yao.

Alisema wahamiaji haramu wengi wao wanaokamatwa ni wale wanaopita wakielekea maeneo mengine, lakini Jeshi la Uhamiaji linaendelea kujizatiti kwa kuziba mianya na maeneo ambayo wakifika wanafanya shughuli nyingine.

Hivi karibuni watu 35 walikamatwa kwenye eneo la Ubena Zomozi, wakidaiwa wahamiaji haramu wakiwa wamejificha ndani ya nyumba.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mafao sawa, kiporo kikokotoo kipashwe moto

**JUZI** Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemevu), Prof. Joyce Ndalichako, akieleza baadhi ya mafanikio ya mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan, madarakani kwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), alisema umelipa mafao yenye thamani ya Sh. trilioni 1.15.

Mafao hayo yamelipwa kwa wastaafu na wategemezi 51,079, huku Sh. bilioni 692.38 za pensheni ya kila mwezi, sawa na wastani wa Sh. bilioni 57.7 kila mwezi kwa wastaafu 147,459.

Hii ni habari njema kwa wastaafu na wategemezi ambao kwa mujibu wa sheria ya hifadhi ya jamii wanastahili kulipwa wanapotimiza vigezo vyote muhimu, lakini kumekuwa na ucheleweshaji kwa sababu ambazo mara nyingi hazijawekwa wazi.

Kilio kimekuwapo pia kwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kwa watu kuchelewa kulipwa mafao yao hasa wastaafu na fao la ukosefu wa ajira, jambo ambalo limesababisha wengi kuishi maisha magumu.

Tunapongeza jitihada zilizofanyika kuhakikisha deni la PSSSF linalipwa, kwa sasa hatutarajii kusikia kilio cha wastaafu kukosa mafao kwa wakati, kwa kuwa wapo waliosota kwa miaka mitatu bila kupata stahiki zao, huku pensheni ya mwezi ikichelewa.

Hivi karibuni, Bunge liliitaka serikali kuweka mikakati madhubuti kulipa madeni kwenye mifuko hiyo, huku wakipongeza kupungua kwa deni la PSSSF, lakini kuitaka mifuko kulipa mafao kwa wakati na kwa mujibu wa sheria.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), ikiwasilisha taarifa ya mwaka 2020/21 ilibaini kuwapo kwa madeni, na kwamba hadi Juni 30, mwaka 2020 deni la serikali la NSSF lilikuwa kiasi cha Sh. trilioni 1.174 ambalo ni la mwaka 2007 hadi 2021.

Pia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), unaidai serikali zaidi ya Sh. bilioni 209.70, hali inayopunguza ufanisi wa mfuko husika na kuharibu mizania ya fedha kinyume na Kanuni za Kimataifa za Uandaaji wa Hesabu.

Mara kadhaa wabunge wametaka kujua hatua zilizofikiwa kwenye utekelezaji wa Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2018, iliyounganisha mifugo na kupata PSSSF, ambayo ilileta kikokotoo chenye usawa baina ya mifuko husika.

Desemba 28, mwaka 2018, aliyekuwa Rais Hayati John Magufuli, aliagiza mifuko kurudi kwenye utaratibu wa awali wa utoaji mafao yaani NSSF kutumia asilimia 25 kukokotoa mafao na pensheni ya mwezi, huku PSSSF wakitumia asilimia 50 hadi mwaka 2023.

Asilimia 25 maana yake ni mtu anapostaafu akipigiwa hesabu ya jumla ya kiasi anachostahili kukipata, mafao ya mkupuo ni asilimia 25 na asilimia 75 inayobakia kwenye mfuko ataendelea kulipwa kama pensheni ya mwezi hadi atakapofariki.

Asilimia 50 maana yake mstaafu anapata kiasi hicho kutoka kwenye jumla kuu, huku akipata asilimia 50 nyingine kama pensheni kwa maisha yake yote.

Iliyokuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Hifadhi ya Jamii (SSRA), ilisema lengo la kuwa na kikokotoo kipya ni kuleta usawa kwa mifuko yote kwa kuwa watumishi wa umma walikuwa wakilipwa mafao ya mkupuo mengi (asilimia 50) huku wa sekta binafsi wanaohudumiwa na NSSF wakilipwa asilimia 25.

Pia walisema kwa mfuko kulipa asilimia 50 ulielemewa kiasi cha kushindwa kuwahudumia wanachama wake na jitihada hizo zilifanyika, ili kuokoa kushindwa kujiendesha kabisa.

Pamoja na mafanikio hayo, lakini bado kuna jambo ambalo ni kiporo linalohitaji majadiliano ya wadau kuhakikisha mifuko inalipa mafao kwa wakati na kuendelea kujiendesha.

Kutokana na hali inayojitokeza kwenye mifuko hiyo ndiyo maana baadhi wameona njia sahihi ni kuchukua michango yao badala ya kusubiri muda wa kustaafu ambao ni miaka 55 kwa hiari na miaka 60 kwa lazima.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Mwaka mmoja wa Rais Samia jinsi anavyojizatiti kukabili vikwazo elimu

**SASA** ni wazi kwamba tatizo la muda mrefu la wanafunzi wa kidato cha kwanza kutoanza muhula wa masomo kwa pamoja kutokana na uhaba wa madarasa limepatiwa ufumbuzi.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, kwa mara ya kwanza mwaka huu, wanafunzi waliochaguliwa kuingia sekondari katika shule mbalimbali za sekondari wameanza masomo kwa pamoja.

Miaka ya nyuma ilizoeleka wanafunzi kuanza masomo ya kidato cha kwanza kwa awamu, sababu kubwa ikiwa ni uhaba wa madaraka uliokuwa ukizikumba shule mbalimbali za sekondari.

Lakini, kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa na serikali ya awamu ya sita, zimechangia kuondoa tatizo hilo, na kilichobaki ni kuweka mikakati ya kuhakikisha uhaba wa madawati unamalizika.

Mikakati hiyo iwe ni pamoja na kushirikisha wananchi ambao kimsingi shule za umma ni zao, hivyo si vibaya wakaendelea kujitolea kuboresha miundombinu ya shule katika maeneo yao ukiwa ujenzi wa madarasa.

Kwa njia hiyo, uhaba wa madarasa unaweza kubaki historia iwapo yatajengwa ya kutosha ikiwamo kuongeza shule mpya ambao kwa namna moja au nyingine zinaweza kupunguza mrundikano wa wanafunzi madarasani.

Wakati huu wa kuelekea mwaka mmoja wa Rais Samia Suluhu Hassan, ni muhimu kukumbushia umma jinsi ambavyo serikali yake imejitahidi kumaliza tatizo la uhaba wa madarasa katika shule za msingi na sekondari.

Kwa mfano, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja, serikali imefanya mengi kwenye sekta ya elimu, ikiwamo kutoa Sh. bilioni 30 kwa ajili ya ujenzi wa shule za sayansi kwa watoto wa kike, katika mikoa 10.

Serikali ametoa Shilingi bilioni 500 kuboresha elimu msingi nchini na amepokea bilioni 304 kupitia mpango wa mapambano na ustawi wa jamii dhidi ya UVIKO-19 huku bilioni 240 kati hizo zikitumika kujenga madarasa 12,000.

Hiyo ni kwa mujibu wa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (anayeshughulikia Elimu), Gerald Mweli, kwamba bilioni 60 zimejanga madarasa 3,000 kwenye vituo shikizi 907.

Katika ufafanuzi zaidi, anasema Sh. bilioni nne zimejenga mabweni 50 ya wanafunzi wenye mahitaji maalum, huku akiongeza kuwa bilioni 113 zimetolewa kujenga miundombinu ya shule za msingi na sekondari.

Anaongeza kuwa kupitia programu hizo, zimejengwa shule mpya za msingi 19 na sekondari 15 kwa gharama ya Sh. bilioni 21.25, huku fedha za tozo ya mawasiliano Sh. bilioni 7 zikitumika kukamilisha maboma ya madarasa 560.

Kwamba, maboma hayo ni ya shule za sekondari yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi katika maeneo mbalimbali nchini, kwa lengo la kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha elimu.

Lakini anataja Mradi wa Kuinua Ubora wa Elimu ya Sekondari Tanzania (SEQUIP), kwamba zimetolewa Sh. bilioni 130.5 kwa ajili ya kujenga shule 214 za sekondari za kata na shule 10 za wasichana za mikoa katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2021/22.

Binafsi ninaona kuna haja ya kufurahia mafanikio hayo katika kipindi cha mwaka mmoja wa Rais madarakani, kuyalinda na kuyaendeleza ili kumaliza kila vikwazo vyote katika elimu.

Ikumbukwe kuwa serikali pia imeruhusu wanafunzi waliokatiza masomo wakiwamo waliopata ujauzito wakiwa shuleni, kujiuliza upya kwa kurejea masomoni ili kutimiza ndoto zao.

Hivyo, kwa uamuzi huo, ni vyema wanafunzi wenyewe watakatumia nafasi hiyo vizuri, huku wazazi na walezi pia wakiwa karibu yao kuhakikisha wanawasimamia watoto wao katika malezi ili waepuka vishawishi.

Rais ameonekana kujipambanua wazi jinsi anavyotamani kila mtoto wa Kitanzania anatimiza ndoto yake katika elimu kwa kuwekeza katika elimu ikiwa ni pamoja na mkakati wa kujenga shule za wasichana katika mikoa 10.

# Tatizo la maji kuwa historia - Mbunge

**Na Joseph Mwendapole**

MBUNGE wa Ukonga jijini Dar es Salaam, Jerry Silaa, amewaahidi wananchi wake tatizo la maji litabaki historia jimboni humo ifikapo mwaka 2023.

Pia amesema ameridhishwa na utekelezaji wa mradi wa maji wa Gongo la Mboto- Chamazi unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

DAWASA kwa ufadhili wa Benki ya Dunia (WB) inatekeleza miradi ya maendeleo ambayo iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji jijini Dar es Salaam.

Silaa aliyasema hayo wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi wa Gongo la Mboto – Chamazi, ambapo alisema ameridhishwa kuona kazi inaenda kwa kasi kwenye maeneo mbalimbali ya Majohe, Gongo la Mboto, Kipunguni, Mombasa, Mazizini, Buyuni, Kinyerezi, Mbondole na mitaa mingine.

Alisema mipango iliyoko ya kuhakikisha huduma ya maji inaimarika katika maeneo mbalimbali ya Jimbo la Ukonga inaridhisha na kutia moyo.

"Kwa mipango iliyowekwa na DAWASA kwenye miradi ya maji na kazi zinazoendelea kutekelezwa sehemu mbalimbali ndani ya jimbo hili, nataka niwahakikishie wananchi kufikia 2023 tatizo la maji Ukonga litabaki historia," alisema Silaa.

"Mimi naamini kwa kazi kubwa inayofanywa na wenzetu DAWASA ya kutekeleza miradi hii ukiwamo mradi wa Bangulo unaosanifiwa, mradi wa Kipunguni, Majohe, Yangeyange na mradi wa Zingiziwa hii itaenda kujibu azma ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kumtua mama ndoo kichwani," alisema.

Silaa aliishukuru serikali kupitia DAWASA kwa kuwezesha upatikanaji wa maji kwenye Jimbo la Ukonga kupitia mtandao wa Ruvu Juu tofauti na awali ambapo walikuwa wakipata maji kutoka Ruvu Chini na kushindwa kufika kutokana na kuwa na msukumo mdogo.

"Niwatake wananchi wa Ukonga kuwa wavumilivu kwa kuwa bado kazi kubwa inafanyika ya kufikisha maji kwenye maeneo yao hatua kwa hatua," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mawasiliano na Huduma wa DAWASA, Neli Msuya, alisema miradi ya nje ya mtandao kazi kubwa inatekelezwa kutoka Gongo la Mboto mpaka Dovya Chamazi na mpaka sasa zaidi ya kilomita tisa za mabomba zimelazwa.

"Mpaka sasa zaidi ya kilomita tisa zimeshalazwa na tunategemea mradi utahudumia wakazi wa maeneo ya Dovya, Mwembebamia, Kisewe na Magengeni," alisema Neli.

Kwa upande wake, Meneja wa usimamizi wa miradi ya Majisafi, Mhandisi Valentine Njau, alisema kazi kubwa inayofanywa sasa ni ya kusambaza maji kupitia miradi hiyo kwa wakazi wa mitaa ya Kichangani, Bombambili na Mbondole.

Alitaja mingine kuwa ni mitaa ya Kipunguni A na B, Mombasa na Mazizini iliyoko kata ya Gongo la Mboto na maeneo mengine ni Kinyerezi Juu na Chini, Buyuni, Mbondole na kwa Mbiki kwenye kata ya Buyuni.

Mradi wa maji Gongo la Mboto - Majohe - Buyuni utahusisha kazi mbalimbali ikiwamo ulazaji wa mabomba ya inchi 10,8,6,4,2 kwa umbali wa kilomita 310 na utakaonufaisha wananchi takribani 59,000.

# Kesi kutishia kuua kwa bastola kuanza Aprili 7

**Na Kulwa Mzee**

KESI ya kutishia kuua kwa bastola inayomkabili mfanyabiashara wa Kariakoo, Adelard Lyakurwa, inatarajia kuanza kusikilizwa Aprili 7, mwaka huu.

Kesi hiyo ilipaswa kuanza kusikilizwa jana katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala mbele ya Hakimu Mkazi Laizer Confort, lakini ilikwama kwasababu hakimu huyo alikuwa na udhuru.

Ilidaiwa mahakamani hapo mbele ya Hakimu Mkazi Nestori Baro, aliyeahirisha kwa niaba na kusema kuwa hakimu anayesikiliza kesi hiyo ana udhuru na shauri liliahirishwa hadi tarehe iliyopangwa kwa ajili ya kuanza kusikiliza mashahidi wa upande wa mashtaka.

Katika kesi hiyo, Lyakurwa anashtakiwa kwa kumtishia kumuua kwa bastola mfanyabiashara maarufu Valence Lekule.

Mshtakiwa anadaiwa kutenda kosa hilo kinyume na kifungu cha 89 (2)(a) cha sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Inadaiwa katika maelezo ya awali kwamba Julai 30, 2020 maeneo ya Kariakoo, mtaa wa Mbaruku na Swahili, Wilaya ya Ilala mshtakiwa akiwa na lengo la kuua, alimtishia Lekule kumuua kwa kutumia bastola huku akijua kufanya hivyo ni kosa la kisheria.

Mshtakiwa anadaiwa kuwa ni mkazi wa Msasani na siku ya tukio la kutishia kuua alikamatwa na kupelekwa Kituo cha Polisi cha Kati kwa tuhuma za kutishia kuua.

Mshtakiwa alikana maelezo yote kuhusu tuhuma zake, lakini alikubali kwamba tarehe iliyotajwa alikuwa maeneo ya Kariakoo, mtaa wa Mbaruku na Swahili na Mei 12, mwaka huu, alikamatwa na kufikishwa mahakamani.

Upande wa Jamhuri katika kesi hiyo unatarajia kuita mashahidi saba.

Mshtakiwa yuko nje kwa dhamana yenye masharti ya kuwa na wadhamini wawili waliokuwa na barua zinazotambulika kisheria na walisaini dhamana ya maandishi ya shilingi milioni moja.



Mafundi wakichimba msingi ikiwa ni maandalizi ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Mshangano inayojengwa katika Mtaa wa Namanyigu, Kata ya Mshangano, Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapatiwa elimu ya bidhaa zenye ubora

**Na Mwandishi Wetu, KIGOMA**

WANANCHI 23,745 wakiwamo wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya za Kasulu, Mlele na Nkasi, wamepatiwa elimu kuhusu umuhimu wa kununua bidhaa zilizothibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Kampeni hiyo ya elimu kwa umma ilimalizika mwishoni mwa wiki kwenye wilaya hizo na ilitolewa katika maeneo mbalimbali ya shule za msingi na sekondari, masoko, stendi na minadani.

Ofisa Masoko wa TBS, Mussa Luhombero, alisema wanafunzi na walimu ni wadau umuhimu wa viwango katika maisha yao ya kila siku, wanapopatiwa elimu hiyo wanakuwa mabalozi wazuri kwenye familia zao na kwa watu wengine.

Kwa mujibu wa Luhombero, elimu hiyo inatolewa kwa wanafunzi na walimu wao ili kuwaandaa kuwa mabalozi wazuri wa kuhamasisha matumizi ya bidhaa zenye ubora ndani ya jamii wanazoishi.

Aliwakumbusha wanafunzi, walimu na wananchi kwa ujumla kutambua vita ya bidhaa hafifu sio ya TBS pekee bali ni ya taifa kwa ujumla.

Luhombero aliwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa wanapokutana na bidhaa zilizokwisha muda wake au wanapotilia shaka bidhaa yoyote katika soko zikiwamo zilizopigwa marufuku kutumika nchini.

Alitolea mfano wa bidhaa zilizopigwa marufuku kutumika kwenye soko la hapa nchini kuwa ni pamoja na nguo za ndani za mitumba, mafuta ya breki na baadhi ya vipodozi vyenye viambata vya sumu.

Luhombero alitoa wito kwa wafanyabiashara kufuatilia taratibu sahihi za usajili wa bidhaa au majengo kupitia mawasiliano waliyopewa pamoja na kutembelea ofisi ya TBS iliyopo karibu au kupiga simu katika kituo cha huduma kupitia mawasiliano waliyopewa.

Baadhi ya walimu na wanafunzi waliopatiwa elimu hiyo walipongeza TBS kwa kutoa elimu hiyo kwa wananchi katika ngazi ya wilaya, kwani itaongeza ufahamu kwa kuhakikisha suala la uuzaji wa bidhaa hafifu sokoni linapungua kama sio kwisha kabisa.

"Niwaombe TBS kuendelea kutoa mafunzo katika vikundi vya wajasiriamali wilayani Lushoto ili waweze kuanza mchakato wa kupata leseni ya kutumia alama ya ubora," alisema mmoja wa wajasiriamali Edward Osward.

# Miili ya mapacha waliofariki dunia yakutwa katika dampo

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WATOTO wachanga ambao ni mapacha, wamefariki dunia wakidaiwa kutupwa katika eneo la kuhifadhia uchafu lililoko Mtaa wa Majengo Makaburini, Kata ya Kambarage Manispaa ya Shinyanga. Tukio hilo lilitokea jana baada ya waokota uchafu kufika kwenye eneo hilo kwa lengo la kutafuta mali na walipofunua moja ya mifuko, walibaini watoto wachanga hao wakiwa tayari wameshafariki dunia.

Mmoja wa wakazi wa maeneo jirani na dampo hilo, Costantine Samweli, alisema kuwa baada ya waokota uchafu kubaini hali hiyo, walipiga kelele zilizosababisha watu wengi kufika kwenye eneo hilo kushuhudia tukio hilo.

"Ukiviangalia vizuri vichanga hivi, huyu mama alivitoa vikiwa bado havijafikisha miezi tisa. Hapa pembeni kama unavyoona kuna sindano na baadhi ya vitu ambavyo vimetumika kumtoa mimba ya watoto hawa," alidai Samweli.

Baadhi ya kinamama waliofika eneo la tukio, kwa nyakati tofauti walikemea kitendo hicho huku wengine wakiangua kilio na kuiomba serikali mwanamke aliyefanya unyama huo na achukuliwe hatua ili kuwa fundisho kwa wengine.

Mwenyekiti wa Mtaa huo wa Majengo, Majid Issa, alisema tukio kama hilo la kutupa watoto wachanga katika dampo hilo ni la pili mwaka huu, akitoa wito kwa wanawake kama mimba zao au watoto wanakataliwa na wanaume, wasiwafanyie ukatili watoto, bali wawapeleke kwenye vituo vya malezi ya watoto.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kuwa wanafanya uchunguzi ili kumbaini mwanamke aliyefanya unyama huo.



Ofisa Miradi Idadi ya Watu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA), Ramadhan Hangwa, akizungumzia umuhimu wa watu kujitokeza kuhesabiwa katika sensa ya watu na makazi, kwenye mkutano wa vyombo vya habari mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Naibu Mwakilishi Mkazi wa shirika hilo, Dk. Ochan Wilfred. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kamati ya Amani kumwombea Rais

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KAMATI ya Amani ya Mkoa wa Pwani inatarajia kufanya kongamano la siku moja kwa ajili ya kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan na taifa ili amani na utulivu viendelee kuwapo nchini.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana mjini hapo, viongozi wa kamati hiyo walisema kongamano hilo ambalo linatarajiwa kufanyika leo mjini Kibaha, litashirikisha watu zaidi ya 200.

Mwenyekiti Mwenza wa Kamati ya Amani, Shekhe Hamis Mtupa, alisema kuwa katika kongamano hilo, mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge.

"Sisi viongozi wa dini wa kamati ya amani tuliketi pamoja tukakubaliana mwezi wa tatu (Machi) ni mwezi wa maombi, kumwombea Rais wetu, kuiombea nchi na kuombea majanga yanayoikabili nchi yetu," alisema.Shekhe Mtupa alisema eneo la kwanza ambalo watafanya ni kuiombea Tanzania kuwa nchi ya amani, huku akihimiza wananchi waendelee kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kuunga mkono jitihada za serikali katika kukabiliana na ugonjwa huo.

Pia alihimiza wananchi kujitokeza kushiriki sensa ya watu na makazi iliyopangwa kufanyika Agosti mwaka huu.

Mchungaji Emmanuel Mhina akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti Mweza wa Kamati hiyo, Beno Kikudo, alisema wameandaa kongamano hilo baada ya kushuhudia juhudi anazozifanya Rais Samia kuijenga nchi bila kukata tamaa.

"Kama viongozi wa dini tumeshuhudia anayoyafanya Rais wetu kwa nchi bila kuchoka wala kukata tamaa, imetusukuma kuandaa kongamano hili kumwomba Mungu amtunze katika kuliongoza taifa letu," alisema.

Mchungaji Mhina alisema watatumia nafasi hiyo kuwahamasisha wananchi ambao hawajapata chanjo ya UVIKO-19, kufanya hivyo kwa afya zao, pia watawakumbusha kuhusiana na umuhimu wa sensa.

Viongozi hao wamesema wanafanya kongamano hilo wakihusisha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia kuwa madarakani.

## Watalii wapongeza maboresho ya msitu

**Na Julieth Mkireri, KISARAWE**

BAADHI ya watalii wa ndani katika Hifadhi ya Msitu wa Pugu Kazimzumbwi ulioko Kisarawe mkoani Pwani, wamepongeza maboresho yanayofanywa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), wakiamini yatashawishi Watanzania kutembelea msitu huo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, watalii hao walisema kwa sasa ukiingia ndani ya hifadhi hiyo, yapo maeneo mengi yametengenezwa kwa ajili ya kupumzikia, pia barabara za ndani za kufikia maeneo ya vivutio zimeboreshwa.

Anna Joseph, mmoja wa watalii waliotembelea katika hifadhi hiyo juzi, alisema anavutiwa zaidi kufika kwenye hifadhi hiyo ambayo ina vitu vingi vya kuvutia.

Mtalii mwingine John Joseph alisema kuwa katika hifadhi hiyo, anavutiwa zaidi na uwapo wa bwawa la asili lijulikanalo kama Minaki ambalo lina samaki wengi, akisifu pia michezo ya kuogelea na kuvua samaki inafanyika huko.

Mhifadhi Misitu wa Wilaya ya Kisarawe, Fred Ndandika kutoka TFS, alisema miundombinu katika Hifadhi ya Pugu Kazimzumbwi inaendelea kuboreshwa.

Ndandika alisema lengo la kuboresha miundombinu ni kuwarahisishia watalii wanapotembelea hifadhi hiyo kufika kila eneo kwa urahisi kujionea vivutio vilivyoko.

Alisema watalii wamekuwa wakiongezeka kutoka zaidi ya watalii 500 mwaka 2019 hadi kufikia 13,000 katika kipindi cha mwaka 2021/22 huku asilimia 70 wakiwa ni watalii wa ndani.

Alisema watalii wa nje walipungua kutembelea hifadhi hiyo kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19, lakini sasa wameanza kufika kutembelea hifadhi hiyo.

Alivitaja vivutio vilivyoko ndani ya hifadhi hiyo kuwa ni pamoja na bwawa lenye kina cha mita nane ambalo halijawahi kukauka na chanzo chake cha maji ni chemchemu na mvua.

Kivutio kingine kilichotajwa ni pango la mzimu, pango la popo, sehemu maalumu ya kupumzikia ya kutafakari na kufanya ibada, miti na kilima ambacho kuna namna ya kukipanda kwa kamba na ukifika kileleni una uwezo wa kuuona Mkoa wa Dar es Salaam kwa asilima 90.

Ndandika aliwahimiza wananchi kutembelea hifadhi zilizoko kwa kuwa kuna mambo mengi ya kujifunza yaliyokuwa yakifanyika zamani.

## Wanufaika na TMA kuboresha uzalishaji

**Na Faustine Feliciane,** KITETO

WILAYA ya Kiteto mkoani Manyara imeanzisha utaratibu wa kushirikiana na wakulima na wafugaji kutumia taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kuboresha shughuli za kilimo.

Uamuzi huo umechukuliwa kutokana na ukame wa muda mrefu ulioikumba wilaya hiyo na kuona umuhimu wa kutumia taarifa za hali ya hewa kwa manufaa ya wananchi.

Akizungumza na Nipashe juzi ofisini kwake, Mkuu wa Wilaya hiyo, Mrakibu Mwandamizi wa Uhamiaji, Mbaraka Batenga, alisema ukame ulioikumba nchi mwaka jana, uliiathiri kwa kiasi kikubwa wilaya hiyo na kuwapa hasara kubwa wafugaji na wakulima.

Alisema kufuatia hali hiyo, Kamati ya Maafa ya Wilaya iliamua kuanzisha utaratibu wa kusambaza taarifa za hali ya hewa za TMA kwa wakulima na wafugaji kwa njia ya simu na mikutano.

"Kwa sasa wilaya yetu kuanzia ngazi ya wilaya mpaka kwa wakulima na wafugaji, tunazifuatilia kwa karibu taarifa zote za TMA kuanzia ule utabiri wao wa siku, wiki mpaka mwezi pamoja na utabiri wa msimu.

"Lengo ni kuwa na tahadhari kwa hali yoyote mbaya ambayo tunaweza kukutana nazo kwenye kila msimu," alisema Batenga.

Aliongeza kuwa alisema wameanzisha makundi ya mtandao wa simu ya 'WhatsApp' kwa baadhi ya wakulima, wafugaji watendaji na wenyeviti wa vijiji wenye simu janja ambao nao wanasaidia kuwapatia wengine wasio na simu hizo taarifa muhimu za hali ya hewa.

"Hii yote inatokana na ukame ambao tulikutana nao msimu uliopita, mazao kunyauka na sehemu nyingine kutoota kabisa, lakini baadhi ya maeneo yetu yanapakana au yapo ndani ya eneo la hifadhi ya asili ya Makame, tumeshuhudia wanyamapori wakifa kwa kukosa malisho na maji," alifafanua Batenga. Alisema kwa wafugaji walipata hasara kubwa ambapo jumla ya mifugo 25,000 ilikufa kwa kukosa maji na malisho kufuatia ukame huo.

Ofisa Wanyamapori wa Wilaya, Dorice Gama, alisema vifo vya wanyamapori na mifugo vilitokana na hali ya kugombania maji yaliyokuwa kwenye mabwawa na visima vichache vya sili kati ya mifugo, wanyamapori na binadamu.

"Hii kwetu imekuwa kama funzo, kwa sasa kuna visima na mabwawa ambavyo vimechimbwa na vimejaa maji msimu huu kutokana na mvua iliyonyesha, hii itasaidia kuwa na uhakika wa maji kwa muda mrefu," alisema Dorice.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya hiyo (Batenga), kwa sasa wilaya hiyo ina mifugo 1,350,000. Kati yake, ng'ombe ni 500,000, mbuzi 480,000 na kondoo 370,000.

# Ujenzi nyumba watakaohama Ngorongoro mbioni kukamilika

**Na Mwandishi Maalumu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali imetenga Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya awamu ya kwanza ya mradi wa ujenzi wa nyumba za wananchi watakaokubali kwa hiari kuhama katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huo inahusisha nyumba 103 ambazo ziko katika hatua mbalimbali. Ujenzi ulianza Februari 28, mwaka huu na hadi kufikia Machi 12, mwaka huu, ujenzi wake umefikia asilimia 78, nyumba hizo zikijengwa katika Kijiji cha Msomera wilayani Handeni mkoani Tanga.

Waziri Mkuu alibainisha hayo juzi alipozungumza na wananchi katika Kijiji cha Msomera kabla ya kukagua ujenzi wa nyumba hizo ambazo kati yake, 53 zimepauliwa na hatua za umaliziaji zinaendelea, nyumba 42 zipo hatua ya boma na nane zipo katika hatua za ujenzi wa msingi.

Alizitaka wizara, taasisi na idara zote za serikali zinazoshughulikia uhamaji wa hiari wa wakazi katika eneo hilo la hifadhi kuendelea kushirikiana kwa karibu ili kukamilisha zoezi hilo kwa ufanisi.

Waziri Mkuu alisema wananchi hao waliokubali kuhama kwa hiari na kwamba watapewa nyumba na eneo lenye ukubwa wa ekari tatu kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao za ufugaji. Wananchi hao wanahama ili shughuli za uhifadhi ziendelee katika eneo hilo.

"Serikali itahakikisha haki zote za binadamu zinazingatiwa katika zoezi hilo la kuwahamisha kwa hiari wananchi wanaoishi kwenye Hifadhi ya Ngorongoro kwenda katika maeneo mbalimbali watakayoyachagua kikiwamo kijiji hicho cha Msomera, ambapo tayari serikali imeshapima viwanja 2,500 na kutenga eneo la ekari 1,700 kwa ajili ya kilimo na malisho," alisema.

Waziri Mkuu aliwaagiza viongozi wa Mkoa wa Tanga wakutane na viongozi wa kijiji na wananchi wa eneo hilo ili waendelee kuwaelimisha kuhusu zoezi hilo na umuhimu wake kwa maendeleo yao na taifa.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema kuwa eneo hilo wamekusudia liwe shamba darasa la ufugaji wa kisasa wenye tija kiuchumi ili kuwasaidia wafugaji nchini wanufaike zaidi na ufugaji wanaoufanya tofauti na ilivyo sasa, hivyo akawaomba watoe ushirikiano kwa serikali yao.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, alitumia fursa hiyo kuwaomba viongozi na wananchi wa Handeni wahakikishe wanasimamia vizuri mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kuepusha migogoro ya ardhi.

"Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za ufugaji yalindwe na yatumike kama ilivyokusudiwa," Ridhiwani aliagiza. Baadhi ya wakazi wa kijiji cha Msomera walisema wako tayari kuwapokea wakazi wa Ngorongoro watakaokubali kwa hiari kuhamia katika kijiji chao, pia walishukuru kwa kuwa ujio wao utakwenda sambamba na uboreshwaji wa miundombinu ya huduma mbalimbali za kijamii kama maji, afya na umeme.

Awali, akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Mratibu wa Mradi, Profesa Wakuru Magigi, alisema umebuniwa kukidhi mahitaji ya kuwa mji wa kisasa wa wafugaji na huduma zote muhimu za kijamii na za wanyama kama majosho na maeneo ya minada zitajengwa.

Alisema wananchi watakaohamia katika eneo hilo watakabidhiwa hati za umiliki wa ardhi ambazo zitawasaidia kupata fursa za kifedha.




Mkurugenzi Mkuu ambaye ni Ofisa Mkuu Mtendaji wa Benki ya NCBA, Margaret Karume, akitoa neno kwa watoto wa wafanyakazi wa Benki ya NCBA walipotembelea benki hiyo katika Siku ya Kimataifa ya Wanawake ikiwa ni sehemu ya kujifunza kimatendo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake viongozi wapewa mtihani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Wanawake wa Mamlaka ya Mapato (TRA) mkoani Dodoma, amewataka wanawake ambao ni viongozi kuonyesha uwezo wao kwenye utendaji kazi pindi wanapopangiwa majukumu, ili kusaidia kuchochea maendeleo kwa jamii.

Fatuma Mshui pia ameitaka jamii kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan za kuleta maendeleo katika nyanja mbalimbali hususani kwenye sekta za elimu na afya.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla yao ya kujipongeza kwa utendaji kazi baada ya kusherehekea Siku ya Wanawake Duniani.

Fatuma alisema wanawake wote, hasa viongozi, hawana sababu ya kubaki nyuma katika kuchangia maendeleo ya nchi.

"Kinachotakiwa ni kuweka jitihada katika kazi wanazofanya, iwe ya ujasiriamali au ofisini, ili kuhakikisha tunasonga mbele na kujiinua kiuchumi kama serikali inavyosisitiza.

"Wanawake hatuna sababu ya kubaki nyuma kwa sababu tunaweza kufanya kazi kwa bidii na kujikwamua kiuchumi na familia zetu," alisema.

Fatuma alisema kauli ya 'wanawake ni jeshi kubwa' lazima ionyeshwe kwa vitendo katika maeneo ya kazi ambayo wamepangiwa kufanya na viongozi.

Alisema kuwa kwa kufanya hivyo, watazidi kuweka msukumo wa kuaminiwa zaidi katika utendaji wao wa kazi za kila siku.

Ezita Kadwela, mtumishi wa mamlaka hiyo, alisema jitihada zilizoko zinaonyesha watafikia usawa wa kijinsia, yaani 50 kwa 50.

Ezita alisema juhudi kubwa zinazofanywa na Rais Samia zinapaswa kuungwa mkono kwa wanawake kuwa mstari wa mbele kufanya kazi kwa bidii na kumwombea ili azidi kufanya mambo makubwa zaidi katika kuleta maendeleo.

# Watendaji wapewa angalizo ujenzi VETA

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, ameuagiza uongozi wa Mkoa wa Simiyu usimamie ipasavyo ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) ili kijengwe kwa viwango vinavyotakiwa kulingana na thamani ya fedha zilizopelekwa.

Kipanga aliagiza hayo jana mkoani humo alipokagua ujenzi wa chuo hicho unaofanyika Bariadi, akisisitiza mradi huo ni wa serikali na fedha zinazotumika ni za walipakodi, hivyo zinapaswa kulindwa ili kuhakikisha zinatekeleza malengo yaliyowekwa.

"Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kupitia Katibu Tawala hapa, mradi huu ni wa kwenu, hivyo ni lazima tuhakikishe tunausimamia kwa ukaribu. Tutengeneze timu ya kazi kuhakikisha tunasimamia kutoka mwanzo mpaka mwisho ili tuweze kuilinda dhamana tuliyopewa ya fedha za walipakodi," aliagiza.

Naibu Waziri Kipanga alifafanua kuwa serikali inajenga jumla ya vyuo 25 vya VETA vya wilaya ambapo katika awamu ya kwanza zilitolewa Sh. bilioni 40 za ujenzi wa vyuo hivyo kwa gharama ya Sh. bilioni 1.6 kila kimoja.

Aliongeza kuwa serikali ilitoa fedha nyingine Sh. bilioni nane kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vya VETA katika wilaya zingine nne na Sh. bilioni nane kwa ajili ya ununuzi wa samani za vyuo vyote 29.

"Hivi tunavyozungumza wilaya 29 tayari kuna vyuo vya VETA ambavyo zaidi ya Sh. bilioni 48.8 zimetumika lakini wilaya zingine vyuo hivyo vilikuwa bado havijakamilika, hivyo Rais alipopata fedha ya UVIKO-19 Oktoba mwaka jana, alisema vyuo hivyo ni lazima vikamilike na kuanza kutoa huduma," alisema.

Awali Mwenyekiti wa Kamati ya Utekelezaji wa Mradi huo, Bazil Gibson, alisema ujenzi wa chuo hicho chenye jumla ya majengo 25, ulianza Februari mwaka huu na unatarajiwa kukamilika Mei mwaka huu, ukigharimu Sh. bilioni 5.1 hadi kukamilika.

Alisema chuo hicho kitakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kwa wakati mmoja, ambapo 320 kati yao watakaa bweni na wengine 180 wa kutwa.

Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Lupakisyo Kapange, alimhakikishia naibu waziri huyo kuwa watasimamia mradi huo ipasavyo ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati uliopangwa.



Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana CCM Wilaya ya Kibiti (UVCCM), Mkoa wa Pwani, Juma Ndaruke akizungumza wakati wa mkutano wa Baraza Kuu uliofanyika wilayani Kibiti. Mkutano huo ulikuwa na lengo la kujadili taarifa ya mwaka 2021 kuanzia Januari hadi Desemba za chama pamoja na mafanikio ya umoja huo kwa miaka mitano iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UVCCM yajivunia mafanikio ya Kibiti

**Na Mwandishi Wetu**

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) wilayani Kibiti mkoani Pwani umepongeza utendaji kazi wa Mwenyekiti wa chama hicho, Rais Samia Suluhu Hassan, ukiahidi kuendelea kufanya kazi naye bega kwa bega ili kukiimarisha zaidi chama chao.

Mwenyekiti wa UVCCM wilayani humo, Juma Ndaruke, aliyasema jana wakati wa kikao cha Baraza Kuu la UVCCM kilichokuwa na ajenda ya kujadili taarifa ya mwaka 2021 pamoja na mafanikio ya umoja huo kwa miaka mitano iliyopita.

"Kwa niaba ya UVCCM Wilaya ya Kibiti, ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa mafanikio yake ya mwaka mmoja madarakani pamoja na kazi kubwa aliyoifanya kwa wilaya yetu.

"Kwa mwaka huo mmoja, ameleta fedha za maendeleo kwa Wilaya ya Kibiti jumla ya Sh. bilioni 2.3 ambazo kwa kiasi kikubwa zimejenga madarasa na kufanya watoto kusoma kwenye mazingira rafiki," alisema Ndaruke.

Aliongeza: "Sisi kama vijana ambao tunapenda maendeleo, tulihakikisha ili kuunga mkono juhudi za Rais Samia, tulishiriki kwa nguvu zote kuhakikisha zinatumika ipasavyo na pia tulikuwa tunajitolea kwenye ujenzi wa madarasa ya watoto wetu kwa kushiriki kwenye ujenzi kama vile kuchimba msingi wa kujenga madarasa."

Kuhusu mafanikio ya UVCCM Wilaya ya Kibiti kwa kipindi cha miaka mitano, mwenyekiti huyo ambaye anamaliza muda wake, alisema uongozi ulioko uliochaguliwa mwaka 2017, ulikuta jumuiya ilikuwa dhaifu kiuchumi kuanzia ngazi ya mashina mpaka wilayani, hali iliyosababisha kukwama kwa utekelezaji wa mipango mingi.

Ndaruke alisema: "Kwa pamoja tuliamua kuweka mpango mkakati wa kuimarisha jumuiya ya vijana kwa wilaya kwa kuweka malengo ya kuamsha hali ya vijana kushiriki shughuli za kisiasa, kuamsha hali ya vijana kushiriki na kujitolea katika shughuli za maendeleo, kuinua hali ya uchumi kwa vijana pamoja na jumuiya na kukisaidia chama kuendelea kuhudumia wananchi na hatimaye kushinda uchaguzi.

"Ninayo furaha kwa siku ya leo kusema kuwa kwa mipango yetu hiyo tulianza kupata matokeo chanya kwani ili kuwapa vijana hamasa, tulianzisha programu ya kambi ya vijana ambapo vijana zaidi ya 500 walishiriki na kunufaika na mafunzo na kutengeneza kikundi cha hamasa kwa vijana na kupata mafanikio ya kushika nafasi ya pili kimkoa kwenye Mbio za Mwenge za mwaka 2021.

"Kwenye kuendelea kuimarisha chama, tuliweza kuzindua mashina mapya zaidi ya 30 katika kata mbalimbali ndani ya wilaya na kusaidia kuongeza idadi ya wanachama na kuimarisha uhai wa chama kwa kiasi kikubwa."

Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, aliyekuwa mgeni rasmi, Kanali Ahmed Abbas, alimpongeza Mwenyekiti wa UVCCM Kibiti, Ndukule, kwa juhudi kubwa za kuwaleta vijana pamoja na kushiriki kwenye kazi za maendeleo na hivyo kufanya kazi ya serikali kuwa rahisi.

Alitumia fursa hiyo kuwaomba wanachama wote wa CCM kujiweka tayari kwa ajili ya uchaguzi wa jumuiya zake ambao unatarajiwa kufanyika mwaka huu.

Wilaya ya Kibiti kwa sasa ina umri wa miaka sita baada ya kurasimishwa mwaka 2016, ikizaliwa kutoka kwenye Wilaya ya Rufiji. Mwaka 2017 uchaguzi wa chama ulifanyika na ndipo uongozi uliopo ulichaguliwa na kufanya kuwa uongozi wa kwanza kwa jumuiya ya UVCCM wilayani humo.

# Mwekezaji atoa mil.100/- kujenga wodi

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MWEKEZAJI wa kampuni ya Foxes Treck kupitia Taasisi yake ya Foxes Community and Wildlife Conservation (FCWC), ametoa zaidi ya Sh. milioni 100 ili kujenga wodi na nyumba ya watumishi katika zahanati ya Kijiji cha Igoda, Kata ya Luhunga wilayani Mufindi mkoani Iringa.

Akizungumza juzi kijijini huko baada ya mfadhili huyo kutembelea kwa lengo la kuona maendeleo ya ujenzi huo, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Igoda, Laines Sanga, alisema kampuni ya Foxes Treck ambao ni wawekezaji wazawa katika kijiji hicho, imeendelea kusaidia shughuli mbalimbali za kimaendeleo, ikiwamo ujenzi wa miradi ya elimu, afya na miundombinu ya barabara ndani ya eneo lao.

Alisema kijiji kinajivunia kuwa na mwekezaji huyo ndani ya eneo lao kwa kuwa pamoja na kufanya shughuli zake za uwekezaji, pia amekuwa nguzo ya maendeleo ya kijiji hicho na vijiji vingine.

"Tunamshukuru sana mfadhili wetu Foxes Treck. Kijiji chetu kilikuwa na changamoto ya ukosefu wa zahanati lakini ametujengea pamoja na kujenga nyumba za watumishi kwenye kituo hiki.

"Wana Igoda wanajivunia sana kuwa na mdau wa maendeleo anayetujali wananchi," Sanga alipongeza.

Muuguzi wa zahanati hiyo, Bahati Ndelwa, alisema uwapo wa zanahati hiyo umesaidia kupunguza vifo vya kinamama wanaokwenda kujifungua kwa kuwa tangu aripoti kituoni huko, hakujatokea kifo hata kimoja kutokana na huduma nzuri inayotolewa kwenye zanahati hiyo iliyojengwa na mfadhili Foxes Treck.

Hata hivyo, muuguzi huyo alisema kikwazo kikubwa ni uhaba wa watumishi kwenye zahanati hiyo ambayo kwa sasa kuna watumishi wawili pekee, hivyo ikitokea mmoja ana tatizo, inamlazimu mtumishi mmoja kufanya kazi zote.

Aliiomba serikali kusaidia kuongeza idadi ya watumishi ili kuboresha zaidi huduma katika zanahati hiyo.

Meneja wa FCWC, Zilipa Mgeni, alisema kampuni ya Foxes Treck imeendelea kusaidia miradi mbalimbali katika kata zote tatu za Ihanu, Mdabulo na Luhunga na kuona vijiji vinavyozunguka kampuni hiyo vinakamilisha miradi ya maendeleo.

Alisema wafanyakazi wa kampuni hiyo wanaupongeza uongozi wa juu wa kampuni kwa kuwa na ushirikiano mzuri na jamii pamoja na serikali kwa kujitolea kutoa huduma kwa jamii pasipo mitafaruku.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Foxes Treck, Geoff Foxes, alisema kampuni yake inatambua umuhimu wa afya bora kwa wananchi wake na ndio sababu ya kujitolea kujenga zanahati hiyo na nyumba za watumishi.

Foxes alisema huduma bora za afya ni pamoja na uwapo wa uzazi wa mpango na kuwa katika zanahati hiyo amejenga chumba cha uzaji wa mpango ili kuunga mkono jitihada za serikali za uboreshaji wa afya.



Ukurasa 12

Ameingilia kati kilio cha makali mikopo kwa wanaosoma elimu juu



Ukurasa 13

Tanzania yaainisha 'jambo lake' kunufaisha teknolojia, sayansi


Nipashe

# TESA

Jumanne Machi 15, 2022

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 14

Ndivyo ilivyo sura kamili ya corona duniani, uso wa WHO unakoangaza

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

## MWAKA MMOJA WA RAIS SAMIA

# Staili yake ya usikivu, akifuatilia kila kikundi



Rais Samia Suluhu Hassan alipotawazwa na kupewa jina la Chifu Hangaya. **PICHA: MTANDAO**

RAIS Samia Suluhu Hassan, wakati huu anapotimiza mwaka mmoja Ikulu, Watanzania wana mengi ya kuzungumza kuhusu majukumu anayoyafanya ambayo wanaona yanaacha alama zisizofutika.

Ikumbukwe Rais Samia, amechukua uongozi wa taifa Machi 19, 2021 kufuatia kifo cha mtangulizi wake, John Magufuli. Mama kama ambavyo wengi wanamuita, amekuwa mstari wa mbele kusikiliza kero za wananchi kwa kualika makundi mbalimbali ndani ya jamii kukutana naye kwa lengo la kusikia vilio vyao.

Juni mwaka jana, anakutana na muhimili muhimu katika jamii wa vyombo vya habari akionyesha kuwa ni msikivu na mchambuzi wa hoja, akifuatilia hatua kwa hatua yale yanayojiri kwenye jamii yanayoufikia umma kupitia vyombo vya habari.

Viongozi wa wana habari wanawasilisha mengi kwa Rais, kuanzia kulipwa madeni ya matangazo yalikaa kwa muda mrefu, kuomba serikali ifanye biashara na vyombo vyote bila kubaguliwa.

Na jingine ni ombi la wahariri wanaopendekeza kuihamishia Idara ya Habari kwenda Wizara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Awali Idara ya Habari ilikuwa kwenye Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, wanahabari wakiona kuwa pengine hapo hapakuwa mahala pake, Rais aliridhia ombi na ushauri huo wa wanahabari, alipoona unafaa kwa maendeleo ya taifa, aliihamisha na sasa kazi inaendelea.

Rais mara kadhaa ameonyesha kiu ya kutaka kusikiliza makundi ambayo anaamini yana umuhimu wa kipekee katika jamii mojawapo ni wazee, vijana na wanawake. Mapema mwezi huu alizungumza na wazee wa Mkoa wa Kusini Unguja, kusikiliza, kuzifahamu na kuzitatua changamoto zao.

Mei mwaka jana alifanya mkutano na wawakilishi wa wazee wote nchini, akikutana kwa niaba yao na wazee wa mkoa wa Dar es Salaam. Lengo lilikuwa kusikiliza na kutafuta ufumbuzi wa changamoto na matatizo yao yanayoibuka baada ya kupokea maoni, vilio na mapendekezo yao.

Ni Rais ambaye hajazisahau sauti za vijana, Juni mwaka jana kwenye uwanja wa Nyamagana mkoani Mwanza ilikuwa zamu yao. Alikutana na vijana kuwasikiliza ili kupanga mikakati ya namna ya kulisaidi kundi hilo kubwa na muhimu ndani ya jamii.

Kama mama anafahamu kuwa vijana wanakabiliwa na ukosefu wa ajira, mitaji ya biashara na pia changamoto nyingi za kumudu maisha yao, wakihitaji serikali iwashike mkono. Lakini anafahamu kuwa ndiyo kundi mhimili wa taifa kwenye siasa, uongozi na nguvukazi, hivyo haliwezi kuwekwa kando.

Kundi mojawapo lenye sauti kubwa kwenye jamii ambalo pia ni wapigakura namba moja ni wanawake.

Rais Samia yuko nao bega kwa bega, Juni mwaka jana alikutana na kuzungumza na wanawake wa mkoani Dodoma kwa niaba ya wanawake wote nchini katika ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Center.

Mengi yanazungumzwa katika ukumbi huo na kubwa ni kutangaza kuwa serikali katika mwaka huu wa fedha, itaanza ujenzi wa sekondari za sayansi mahsusi kwa wasichana katika mikoa yote.

Anawaahidi kinamama kuwa pamoja na jitihada hizo usawa wa kijinsia ni suala ambalo linapewa kipaumbele na kwamba uteuzi unaozingatia utaratibu wa 50/50 kwenye ngazi mbalimbali za uongozi na vyombo vya kufanya maamuzi haukwepeki.

Viongozi wa dini ni kundi lenye ushawishi mkubwa na muhimu katika taifa, ndiyo walezi wa roho za waamini kwenye nyumba za ibada na ambao wanakubalika na wale wanaowaongoza.

Rais anakutana na viongozi wa dini mbalimbali hivi karibuni na kusikia kilio chao, ushauri na mapendekezo wanayoamini ni muhimu kwa maendeleo ya nchi kwenye kuhakikisha usawa, amani na upendo nchini.

Katika mkutano huo, viongozi wa dini wanamwomba kumwachia huru Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wanachama wengine watatu waliokuwa wameamuliwa na mahakama kuwa wana kesi ya kujibu katika mashtaka ya ugaidi yaliyokuwa yanawakabili.

Ni katika kesi iliyofunguliwa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. Rais aliridhia ombi lao na ilipofika Ijumaa Machi 4, 2022 Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Sylvester Mwakitalu, iliwasilisha ombi mahakamani ikieleza kuwa haina nia ya kuendelea kusikiliza shauri hilo na ukiwa mwisho wa gumzo la kuachiwa Mbowe lililokuwa linawasilishwa kwa serikali kila wakati.

Septemba mwaka jana, Watanzania wanashuhudia Rais Samia, akipewa jina la 'Hangaya'. Anapokea heshima ya kuwa Hangaya ikimaanisha Nyota Angavu na Mkuu wa Machifu au viongozi wote wa serikali na mila nchini.


INAENDELEA UK.14

NA SABATO KASIKA

# Ameingilia kati kilio cha makali mikopo kwa wasomao elimu juu

• Ahueni; yafutwa riba asilimia 15 • Kigezo kipya; kila aliyejiunga chuo



Wanafunzi wa Chuo Kikuu Mzumbe, walipokusanyika kumsikia Rais Jakaya Kikwete ( sasa mstaafu), alipozuru chuoni hapo. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

JUMAMOSI wiki hii, Rais Samia Suluhu Hassan atatimiza mwaka mmoja tangu aapishwe kuwa Rais wa Tanzania, Machi 19 mwaka 2021, baada ya kifo cha mtangulizi wake John Magufuli.

Katika kipindi hicho, tangu ameingia madarakani, yapo mengi ambayo serikali yake imeyafanya kwa ajili ya maendeleo ya nchi na yamekuwa yakizungumzwa na watu wa kada mbalimbali wanaohojiwa na vyombo vya habari.

Wiki hii Nipashe imezungumza na baadhi ya watu ambao wameelezea jinsia wanavyouona mwaka mmoja wa Rais Samia madarakani na kile ambacho serikali yake imekifanya kwenye elimu.

Mmoja wa wadau wa elimu, Magdalena Sakaya anasema, mwaka mmoja wa Rais Samia, umeleta neema katika sekta elimu ikiwamo kufuta asilimia 15 ya riba ya mikopo kwa wanafunzi waliohitimu chuo kikuu, waliyokuwa wanatozwa baada ya kuhitimu.

"Wahitimu walikuwa waliopata mkopo walikuwa wanaumizwa na asilimia hiyo ambayo kwa muda mrefu walilalamika sana. Ni furaha kwao baada ya mama kuiondoa. Hii ni neema kwa wahitimu na wanaoendelea na masomo," anasema Sakaya.

Anataja kingine ambacho Rais amekifanya kuwa ni ujenzi wa madarasa ya kutosha katika shule za msingi na sekondari hali iliyochangia kutokuwapo kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza kuanza masomo kwa awamu.

> "Kumnyima mtoto wa kike au wa kiume, ni miongoni mwa vitendo ambavyo huchukuliwa kama ukatili wa kijinsia, ambao kituo chetu kinapambana navyo kwa kuelimisha jamii ili ibadilike.

"Yaani, pesa za UVIKO-19 alizopata kutoka kwenye mashirika ya fedha amezitendea haki, ni vyema tumpongeze katika hilo, kwani pesa hizo zimesaidia angalau kupunguza msongamano wa wanafunzi wetu madarasani," anasema.

**ELIMU BURE IMEIMARIKA**

Janeth Mawinza, Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), anasema, mwaka mmoja wa Rais Samia, sera ya elimu bure kwa shule za msingi na sekondari imezidi kuimarika na kung'ara.

"Kama unakumbuka, mtangulizi wake alianzisha sera hiyo, wanafunzi wakawa wanaandikishwa wengi, lakini wanakosa madarasa shuleni, lakini sasa kipindi cha mwaka mmoja yamejengwa mengi," anasema Janeth.

Aidha, anasema, hata ufaulu wa kuingia sekondari kwa watoto wa kike umeongezeka na pia hatua ya serikali kuruhusu wanafunzi waliopata ujauzito kurudi shuleni kuendelea na masomo inazidi kuimarisha usawa wa kijinsia kwenye elimu.

"Tunakwenda vizuri kuleta usawa wa kijinsia katika elimu, ila bado kidato cha sita kwenda chuo kikuu, wanafunzi wa kike wanaofaulu kwenda huko ni wachache, si sawa na wale wa msingi kwenda sekondari," anasema.

Anasema, Rais anapotimiza mwaka mmoja madarakani, yapo mengi ya kujivunia kwa upande wa elimu, kwamba uandikishaji wa watoto katika elimu ya msingi umekuwa na uwiano, wasichana wengi wanaandikishwa.



Mkuu wa Bodi ya Elimu ya Juu, Ablu-Razak Badru.

"Umekuwa mkombozi kwa wasichana wengi waliositisha masomo au kutojiunga kutokana na uhaba wa fedha na mila potofu, hivyo kila Mtanzania hana budi kujivunia mwaka mmoja wa Rais wetu," anasema.

**TUKO VIZURI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kiota Women Health Development (KIWOHEDE), Justa Mwaituka, anasema, mwaka mmoja wa Rais Samia, umekwenda vizuri ingawa bado kuna changamoto kwenye elimu.

"Taasisi ya Haki Elimu, inaeleza kuwa kwa sasa kuna uwiano sawa kati ya watoto kike na wa kiume wanaoandikishwa kwenda shule, lakini watoto wa kike wanakumbana na vikwazo mbele ya safari," anasema Justa.

Anaongeza kuwa wanapopevuka wanakutana na vishawishi ambavyo wakati mwingine vinakwamisha ndoto zao kwenye elimu, na kwamba hata wakienda sekondari, huko nako wanakutana na vikwazo vingine.

"Unakuta shule za sekondari ziko mbali, wanalazimika kutembea umbali mrefu tena njiani wanakumbana na vishawishi vinavyoweza kuwaingiza katika mahusiano ya kimapenzi na kujikuta wakipata mimba," anasema Justa.

Justa anasema, umbali huo wa shule, husababisha baadhi ya wanafunzi kupanga katika nyumba za mitaani kutokana na ukosefu wa mabweni, na kwamba mazingira kama hayo pia si salama kwao.

"Hivyo wito wangu wakati huu wa mwaka mmoja wa Rais wetu ni kwamba, serikali na wadau wake iangalie uwezekano wa kumaliza vikwazo hivyo kwa mtoto wa kike katika elimu," anasema.

**VIKWAZO VINAPUNGUA**

Mwenyekiti wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni Dar es Salaam, Fatma Talib, anasema, vikwazo kwa mtoto wa kike kupata elimu vikiwamo ukeketaji ndoa na mimba za utotoni vinazidi kupigwa vita.

"Kituo chetu kinashughulika na vita hiyo, kwa hiyo tunaona jinsi hali ilivyo kwani tumesaidia baadhi ya wasichana wanaokimbia ukatili huo na kuwaleta kituo chetu kuwapa elimu ya ufundi ili wajitegemee," anasema Fatma.

Anasema, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja wa tangu Rais Samia, aingie madarakani, kumekuwapo na kasi ya kukabiliana na vitendo vya ukatili vinavyochangia kumnyima elimu mtoto wa kike.

"Kumnyima mtoto wa kike au wa kiume, ni miongoni mwa vitendo ambavyo huchukuliwa kama ukatili wa kijinsia, ambao kituo chetu kinapambana navyo kwa kuelimisha jamii ili ibadilike," anasema.

Mwenyekiti huyo anasema, pamoja na mafanikio yaliyoko, bado jitihada zaidi zinahitajika ili kuhakikisha vita ya kukomesha vitendo vya ukatili katika jamii vinavyochangia kumkwamisha mtoto wa kike kielimu vinaisha nchini.

NA JENIFER GILLA,
ALIYEKUWA KIGALI

KUTOKA DARASA LA STI KIGALI

# Tanzania yaainisha 'jambo lake' kunufaisha teknolojia, sayansi

• Maonyesho ubunifu kuwa kila mwaka

JIJINI Kigali nchini Rwanda, unafanyika mkutano wa kanda wa Afrika kujadili mafanikio, changamoto na mikakati ya kufanya ili kufikia malengo ya maendeleo endelevu (SDGs) mwaka 2030.

Ni tukio lililoanza Machi 4 hadi 5, mwaka huu, mkutano ukiangazi namna nchi za Afrika zinavyohitaji kukuza Sayansi, Teknolojia na Ugunduzi (Science, Technology and Innovation-STI), ili itumike kukuza uchumi na kuongeza kasi ya kufikia ajenda ya 2030 ya maendeleo endelevu.

Aidha, kuwezesha kufikia Ajenda ya the 'Africa We Want - Agenda 2063' au 'Afrika Tunayoitaka ya mwaka 2063' inayopigiwa chaguo na Umoja wa Afrika (AU).

Katibu Mtendaji wa Uchumi Tume ya Afrika (ECA), Vera Songwe, katika ufunguzi wa kongamano la nne la Sayansi, Teknolojia na Ugunduzi, jijini Kigali, anaagiza kuanzishwa Maendeleo ya Teknolojia ya Kiafrika na Mtandao wa kuchochea uvumbuzi na kuharakisha maendeleo.

"Tunahitaji kujenga misingi sahihi ya kisayansi, kiteknolojia na uvumbuzi ili kuleta majibu ya haraka, kama ilivyoshuhudiwa karibuni, nchi zetu nyingi zilihitaji msaada kupima COVID-19, ulikuwa utegemezi zaidi wa kwenye vifaa vya matibabu kutoka Ulaya. Afrika inahitaji kukuza sekta hii hasa uvumbuzi kupunguza utegemezi wa aina hii," anasema Vera.

### KUTOKA TANZANIA

Kauli ya Tanzania kwenye kongamano zilizofanya kukuza sayansi, teknolojia na ugunduzi, kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), wataalamu wengi wameshaelimishwa.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, katika mkutano ndani ya mjumuiko huo wa Kigali, kwamba wataalamu wamejengewa uwezo wa matumizi ya STI kwenye masuala mbalimbali.

Waziri Saidi anasema mafunzo yanaendelea pamoja na mapitio ya muswada wa Sheria ya Tume ya Kitaifa ya Sayansi na Teknolojia ya 2000, lakini mengine yanayofanywa ili kufungua njia ya kukuza STI nchini ni kupitia Sera ya Taifa ya STI ya 1996 na Sheria ya Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ya 2000.

Aidha, anataja ushiriki katika matukio yenye mrengo wa kukuza STI kama Wiki ya Sayansi au Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana katika sayansi iliyofanyika Februari 11, mwaka jana na huu," anasema, akigusia Mei 2022, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia inatarajia kuandaa Wiki ya Kitaifa ya Ubunifu.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said (katikati), akifafanua mpango wa Tanzania katika kukuza sayansi na teknolojia, katika mkutano wa nane wa Afrika wa Maendeleo Endelevu uliofanyika jijini Kigali, Rwanda, siku chache zilizopita. **PICHA: JENIFER GILLA**

> "Novemba, 2021 UNESCO iliwezesha kutoa mafunzo kuhusu sera na nyenzo ya sayansi nchini ili kuwawezesha kubuni sera ya STI zinazoendana na Agenda ya AU ya mwaka 2063.

### MAFANIKIO YALIVYO

Waziri anasema, hado sasa nchini mambo kadhaa yamefanyika kama kuimarisha uelewa wa haki za binadamu, kupinga ubaguzi na uhuru wa kisayansi katika sera ya sayansi.

Anafafanua, mfumo umeshakuza ushirikiano wa jumuiya ya wanasayansi na kuzingatia masuala yaliyo nje ya utafiti wa chuo kikuu.Taarifa za UNESCO zinaonyesha kuwa uwekezaji wa kimataifa katika utafiti maendeleo (R&D) una uhusiano chanya na mkubwa, pia kukua pato la taifa.

Anatoa mfano, Korea Kusini inatumia takriban asilimia mbili ya pato la taifa kwa utafiti wa sayansi, teknolojia na ubunifu, ilhali Afrika Kusini, inatumia kati ya asilimia 0.5 hadi 0.9 ya pato la taifa.

### UJUMUISHAJI NI MUHIMU

UNESCO inasema ili kukuza STI na kuitumia katika uchumi na ujumuishi ni lazima, kama shirika hilo linavyoshirikiana na mataifa ya Afrika, kuhakikisha teknolojia na sayansi inatumiwa kuleta maendeleo.

"Mfano watafiti wanapomaliza kazi na kuweka matokeo mezani, inahitajika timu ya kuyajadili, kisha kugawanya majukumu ya kufanyia kazi utafiti huo katika makundi mbalimbali.

"Wazo hili la STI lazima ligawanywe kwa wakurugenzi wote wa serikali ndani ya wizara ili nao waweze kuzungumzia hoja hiyo na watendaji wao, ili wapange watatumia njia gani kubuni mikakati," ni kwa mujibu wa Waziri Said.

Anasema Wizara ya Elimu, ina jukumu la kuanza kupitia mitaala na kuibadilisha kuwajengea uwezo wa wanafunzi wa STI, ili wawaelekeze watoto kuwa wabunifu.

Vyuo vikuu navyo, Jumuiya ya Afrika Mashariki nayo inahitaji kuchukua nafasi yake katika hili kwa kushindanisha wanafunzi wa elimu ya juu, katika ukanda huu, ili kuendeleza na kukuza ubunifu miongoni mwao.

Hoja ya ushirikiano iliungwa mkono na Mkurugenzi wa UNESCO wa Afrika Mashariki, Hubert Gijzen, anayeiambia Nipashe kwamba bila ya kuwa na ushirikiano wa Afrika, suala hilo halitafanikiwa.

"Tunahitaji ushirikiano wa kisayansi huria kati ya nchi. Ndiyo maana UNESCO ilizindua mfumo huria wa kisayansi mbayo nchi wanachama 193 zimeuidhinisha," anatamka Gijzen.

Kwenye ushiriki wa Tanzania, anasema mkutano una manufaa makubwa, kwa vile inapata nafasi ya kujifunza kwa wengine waliyofanya hadi kufanikiwa.

### WADAU WENGINE

Waziri wa Elimu wa Rwanda, Valentine Uwamariya, anasema jukwaa la STI litatoa njia zitakazosaidia sayansi na teknolojia ya Afrika, kufikia malengo yao chini ya muongo mmoja.

"Mpango Mkuu wa Kitaifa wa TEHAMA na Elimu wa Rwanda ni kukamilisha juhudi za kueneza mageuzi ya teknolojia ya mawasiliano ya simu- 4G nchini. Hii ilikuwa ni moja ya mipango ya kuwaandaa wanafunzi ili kukidhi mahitaji ya kimataifa ya TEHAMA." Anafafanua.

Naibu Mtendaji Katibu Mkuu na Mchumi Mkuu wa Jukwaa la Uchumi wa Afrika (ECA), Hanan Morsy, anashauri kufanyiwa kazi kwa hitaji la kukuza TEHAMA ili kukidhi mahitaji ya soko huria.

"Ni asilimia 20 tu ya wahitimu wa Afrika wanasomea TEHAMA. Lakini kuna ongezeko la uhitaji kutoka masoko ya kazi hiyo. Sekta za elimu hazijabadilika. Tumeona hii katika nchi ambazo wamefanikiwa na STI Korea Kusini Korea na China," anasema.

Mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Msingi Zawadi, Janeth Mwaimu, anasema somo la sayansi, teknolojia na ubunifu linapaswa kupewa kipaumbele hata kwa shule za sekondari ili kuendelea kukuza vipaji yao, kwami kwa sasa hayao sekondari.

### CHANGAMOTO

Baadhi ya changamoto zinazoonekana kuirudisha Tanzania nyuma katika kukua kiteknolojia ni uchache wa watafiti.

Ripoti ya Tume ya Sayansi na Teknolojia-(COSTECH) ya 2018 inaonyesha uwiano wa idadi ya watafiti nchini ni 60 kwa kila watu 1,000,000, hivyo ni vigumu kupata matokeo ya utafiti kuwezesha ma lengo ya kuundwa bidhaa mpya, taratibu na huduma zake.

Rpoti inaeleza kuwa utafiti juu ya mifumo ya uvumbuzi katika nchi zilizochaguliwa za Kiafrika (NEPAD, 2009) ikijumuisha Uganda na Tanzania zimeonyesha kuwa kuna idadi ndogo ya wataalamu wenye sifa za kiufundi kufanya shughuli za uvumbuzi katika viwanda.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Ndivyo ilivyo sura kamili ya corona duniani, uso wa WHO unakoangaza

WAKATI dunia inaingia katika mwaka wake wa tatu tangu ugonjwa wa Covid-19 kutangazwa kuwa janga la ulimwengu, je, ni kwa kiasi gani janga hilo limeathiri maisha ya watu ulimwenguni kote?

Ugonjwa wa Covid-19 unatajwa kugharimu maisha ya zaidi ya watu milioni sita duniani kote. Wataalamu wanakadiria idadi hiyo huenda ikawa mara mbili au mara nne zaidi ya iliyoripotiwa, huku vifo vingi vikiripotiwa zaidi miongoni mwa wazee.

Na kwa wale walionusurika kifo baada ya kuugua, wanaendelea kupambana na athari za muda mrefu za ugonjwa unaoshambulia mapafu na wengine, wameachwa na ulemavu wa kudumu kutokana na ugonjwa huo wa Covid-19.

**WANAFUNZI WALIOKOFIKIA**

Ugonjwa wa Covid-19 unatajwa kuzima ndoto za wanafunzi wengi kielimu, takriban ikiwagusia wanafunzi bilioni mbili na safari yao ya elimu imefika mwisho ghafla.

Shule kadhaa nazo zililazimika kufungwa na kusitisha elimu kwa mamilioni ya wanafunzi hasa wasichana na watoto maskini. Hali hiyo iliwasukuma wasichana wengi ndani ya shimo la ndoa za mapema, ilhali wengine walianza ulezi au uzazi kabla ya kubalehe.

Pia janga la Covid-19 ilitarajiwa imekuwa sumu kwa maendeleo kimataifa na takwimu zinaonyesha kuwa watu nusu bilioni walilazimishwa kuingia katika umaskini, na wale waliokuwa maskini tayari, hali yao ya umaskini ilizidi kuwa mbaya na mpaka sasa, janga limesababisha kudorora kwa uchumi duniani kote.

Wakati dunia inaingia katika mwaka wa tatu wa janga hilo kidunia, mwanya wa ukosefu wa usawa umezidi kupanuka na mfano hai ni katika usambazaji wa chanjo dhidi ya virusi vya corona.



Baadhi ya wanafunzi wa nchini India, wanaosomea nje ya darasa kukabili hatari ya maambukizi ya corona. **PICHA: MTANDAO**

> WHO imetoa mwito kwa mataifa ya Ulaya kuzingatia zaidi suala la afya kuliko ilivyokuwa kabla ya janga la virusi vya corona.

Nchi maskini nazo zinaelezwa kuwachwa nyuma katika kasi ya chanjo. Kutimu miezi 15 baada ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kuidhinisha chanjo ya kwanza dhidi ya Covid-19, kumetokea tofauti kubwa katika usambazaji wa chanjo hiyo.

Ni dhahiri zipo sehemu ambazo watu wanapokea dozi ya tatu au hata ya nne ilhali zaidi ya asilimia 85 ya watu wanaoishi katika nchi za kipato cha chini bado wanasubiri angalau dozi ya kwanza tu za kuwapa matumaini ya kupambana na ugonjwa wa Covid-19.

Licha ya kutolewa chanjo, kunatajwa mkoko ndio mwanzo unaalika maua katika maeneo dunia bado inajikuna kichwa, ni nini kilipaswa kufanyika tofauti na kupambana na janga hili?

Utafiti wa Taasisi ya Human Rights Watch, umeangazia miongoni mwa sababu za janga la Covid-19, limeonekana kukosa mwarobaini. Mojawapo ni kushindwa kwa serikali kulinda haki za binadamu na kutumia janga la Covid kama mbinu za kupanua mamlaka na hatimaye kuzima upinzani.

Human Rights Watch inapendekeza mbinu mbadala za kuzingatiwa iwapo kweli dunia inataka suluhu ya kudumu kupambana na jinamizi hili la Covid-19.

**KUTOKA UJERUMANI**

Kuna maoni Ujerumani inatumia kuidhibiti Omicron, lakini Waziri wake wa Afya, Karl Lauterbach anatahadharisha kwamba si sahihi wito wa baadhi ya wanasiasa wa upinzani wanaotaka hali ya sasa ya vikwazo vya corona iondolewe nchini humo.

WHO nayo imetoa mwito kwa mataifa ya Ulaya kuzingatia zaidi suala la afya kuliko ilivyokuwa kabla ya janga la virusi vya corona.

Aina mpya ya kirusi cha Omicron inaripotiwa kusambaa katika nchi za Denmark, Uingereza, India, Sweden na nyingine nyingi, hata hivyo athari ya mabadiliko yake haipo wazi sana.

Wabunge kadhaa nchini Kenya wanatajwa kuambukizwa kirusi cha corona cha Omicron na WHO inaonya kuwa "kuongeza chanzo zaidi za kuimarisha kinga kutaongeza tatizo cha covid-19.'

Serikali ya Ethiopia, nayo inadai kukomboa mji katika mkoa wa Tigray na Marekani, yaruhusu maofisa wake na UN kushirikiana na Taliban katika biashara rasmi.

**Kwa mujibu wa Mtandao**

## Mwaka mmoja wa Rais Samia; staili yake usikivu, akifuatilia kila kikundi

**INATOKA UK.11**

Ni baada ya kukutana na Umoja wa Watemi na Machifu wa Kisukuma wanaoshirikiana na Umoja wa Machifu wa Tanzania.

Rais anapewa jina 'Hangaya' au Nyota Angavu, na kwamba yeye ndiye mkuu wa mamlaka zote nchini, hatua inayoonyesha kuwa anawakubali viongozi wa mila na kuheshimu sauti zao kwenye kuchochea maendeleo na kubadili mabaya kwenye jamii ili kupata maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mtemi Kiongozi wa Sukuma, Aaron Mikomangwa anafafanua kuwa watemi wametambua mchango wa Rais Samia kwenye uongozi unaothamini na kuheshimu haki za wanyonge, kulinda na kuthamini utamaduni wa Watanzania.

Rais ambaye ni mama anaendelea na jukumu la kuwasikiliza Watanzania na huenda kazi itaendelea kuwasikiliza wadau wa makundi mengine kwenye maeneo mbalimbali, kulingana na ratiba na shughuli zake.





# Serikali kushirikiana na jamii kukomesha mauaji ya wazee

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, amekerwa kuendelea kuwapo kwa mauaji ya wazee kwa kisingizio cha uchawi na kudai kuwa serikali imejipanga kukomesha vitendo hivyo kwa kushirikisha jamii na viongozi wa dini.

Dk. Gwajima aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizindua Baraza la Taifa la Wazee kwa kushirikiana na Mtandao wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali Tanzania, uliofanyika jijini hapa.

Alisema juhudi za serikali zimefanya kazi kubwa ya kupambana na mauaji jambo ambalo takwimu zinaonyesha kuwa yamepungua kutoka wazee 190 mwaka 2015 hadi kufikia 54 mwaka 2020 na kuwa takwimu hizo hazimfurahishi.

"Bado watu 54 wanauawa ni watu wengi, kuendelea kwa mauaji ya wazee kwa kisingizio cha uchawi kutokana na kuwa na macho mekundu, huu uchawi wanauona wao tu, ni lazima tuikomeshe hali hii na tutashuka hadi chini kwa kushirikiana na jamii na viongozi wa dini," alisema.

Kuhusu huduma za afya kwa wazee, Dk. Gwajima alisema serikali itahakikisha inakuwa na kanzidata ya wazee kupitia mabaraza yao na kuondokana na kadhia ya wazee ya kuishia kuwa ombaomba barabarani.

"Mabaraza yatakuwa na kazi ya kufuatilia wazee katika maeneo yao maana ni aibu kwa wazee kuwa barabarani wakiombaomba, tunatakiwa wafahamike na wale wenye uwezo wawajibike kuwalewa wazee na wale wasio na uwezo serikali itaangalia namna ya kuwatunza na hii itaondoa wazee kuombaomba barabarani," alisema.

Kadhalika, alisema ili kukabiliana na upunguzu wa Maofisa Ustawi wa Jamii, wizara yake inaomba nafasi za ajira kwa kada hizo. Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, alisema wazee ni tunu ya taifa ni muhimu kuwapo kwa baraza hilo ili kusaidia kuwapo kwa maadili kwa jamii.

Alisema serikali imejikita kuboresha makazi ya wazee ili kuwatunza ambao hawatakuwa na watu wa kuwatunza huku akisisitiza kukutana na mashirika 13 ambayo yamesajiliwa kushughukulikia masuala ya wazee ili yatimize wajibu wao.

Awali Mwenyekiti wa Baraza hilo, Lameck Sendo, aliiomba serikali kutunga sheria ya wazee kwa kuwa Sera ya Wazee ya Mwaka 2003 imekuwa ya muda mrefu.

Naye Mwenyekiti wa Mtandao wa Wazee, Clotilda Kokupima, alisema mpaka sasa mabaraza ya wazee 47,876 yameanzishwa.

# Waziri aagiza kuundwa timu ufumbuzi upatikanaji vitabu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amemwagiza Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa, kuunda timu ndogo itakayosaidia kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la upatikanaji wa vitabu nchini.

Hatua hiyo ilifikiwa juzi na Waziri Mkenda jijini hapo kwenye mkutano wa wadau wa vitabu uliokutanisha wachapishaji, wasambazaji na waandishi wa vitabu nchini baada ya kusikiliza hoja mbalimbali kuhusu upatikanaji wa vitabu.

Aliagiza timu hiyo ishirikishe Chama cha Wachapishaji nchini (PATA) na Chama cha Wauza Vitabu Tanzania (BSAT) ili suala la upungufu au uhaba wa vitabu liwe la kihistoria.

Prof. Mkenda alisema serikali itakuwa tayari kupokea mapendekezo yatakayowasilishwa na timu hiyo ili vitabu vipatikane kwa wingi nchini na kuamsha hali ya usomaji vitabu.

Alisema kuwa wachapishaji wa hapa nchini wanapaswa kujengewa uwezo ili kuondokana na kutumia gharama kubwa kuchapisha vitabu nje ya nchi.

"Suala la printing ni tatizo wakati mwingine tufanye maamuzi magumu, tuna wachapishaji hawana uwezo mkubwa, lakini akijua anapewa kazi anaweza kuchukua mkopo benki tukiendelea kwenda India au Dubai hawa wa nchini hawatawekeza maana nani atakwenda kuchapisha, pia taasisi za umma," alisema.

Aidha, aliitaka TET kutafuta ufumbuzi wa kudumu ili kuondokana na tatizo lililojitokeza mwaka huu la kuchelewa kwa vitabu vya kiada hususan vya darasa la saba.

"Nasema kweli tumeboronga, sitaki kusikia upungufu wa vitabu ambavyo tumeandika wenyewe, kwa mfano NECTA (Baraza la Taifa la Mitihani) walikuwa wanachapisha nchini Uingereza na ilipotokea janga wakaamua hawatakwenda kuchapisha tena na hivi sasa wanachapisha wenyewe," alisema.

"Tunapozungumza ubora wa elimu ya nchi yetu ni pamoja na kuhimiza watu kusoma na kama kuna mtu yeyote anazuia vitabu visisomwe huyo anachangia kudidimiza hata kama tukibadilisha mitaala mara 100 haitasaidia kama tutazuia watu kusoma vitabu mbalimbali."

Alisema hakuna ofisa yeyote ambaye ameagizwa kuzuia vitabu au kuwatisha wauzaji wa vitabu na kutaka viuzwe vya Taasisi ya Elimu nchini (TET) pekee.

"Sisi kinachofanyika kuna vitabu ambavyo vimeidhinishwa na kimechukuliwa kama kitabu kiongozi ambacho mwalimu akiwa anafundisha atakitumia hilo ni sharti, pia kuna vitabu ambavyo vimepata ithibati ambavyo ni vitabu vya ziada mwalimu ana wajibu wa kuhimiza wanafunzi au wazazi kuvinunua ili kusaidia zaidi, lazima hili tulifanye," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa TET, Dk. Aneth Komba, alisema vitabu vilivyokwenda kuchapishwa vya madarasa mbalimbali vitaingia leo nchini ili kuondoa upungufu uliopo huku akiahidi kushughulikia hoja zote zilizoibuliwa na wadau kwenye mkutano huo.

Awali, muuzaji wa vitabu kutoka kampuni ya Nice Enterprises, Stanely Nzovu, alisema tangu Desemba mwaka jana hana vitabu vya kiada vya darasa la saba na baadhi ya masomo darasa la pili, la nne na la tano na kuomba serikali kuondoa tatizo hilo na kuongeza vyanzo vya upatikanaji vitabu badala ya kutegemea TET pekee.

Mwenyekiti wa PATA, Gabriel Kitu, alidai kuwa baadhi ya wadhibiti ubora wamekuwa wakikataza wanafunzi na wazazi kununua vitabu ambavyo havizalishwi na TET jambo ambalo linaua soko.

Mwenyekiti wa BSAT, Albert Mwaipyana, aliomba serikali kushughulikia kero zinazoikabili sekta ya vitabu ili kuimarisha soko nchini.



Mkazi wa Kijiji cha Bahi, Edward Matonya, akichota maji katika Mto Bubu kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, juzi mkoani Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watumishi H/shauri Chemba watakiwa kujitafakari

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka watumishi wa Halmashauri ya Chemba kujitafakari kwenye utumishi wao kutokana na kuchangia halmashauri kurudi nyuma kimaendeleo.

Mtaka aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na watumishi wa halmashauri hiyo na kusikiliza kero zinazochangia kusuasua katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo.

Alisema Chemba imekuwa na kiwango cha chini katika ufaulu na miradi mbalimbali ya maendeleo kutotekelezwa kwa wakati na hiyo inatokana na uwapo wa malumbano yasiyokuwa na msingi katika maeneo ya kazi.

Alimtaka mkurugenzi wa halmashauri hiyo kupembua na kuangalia kwa makini ushauri anaopewa na baadhi ya watumishi.

Kadhalika, aliagiza kushughulikiwa suala la watendaji wa vijiji na kata kubambikiziwa madeni kutokana na hitilafu ya mifumo ya mashine ya kukusanyia mapato.

Alikitaka kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kufanya uhakiki wa mashine hizo na kubaini kama zina kasoro ili zirekebishwe.

Kuhusu sekta ya elimu wilayani humo, Mtaka alisema wadau wa elimu wanapaswa kubuni mbinu zitakazosaidia kuinua kiwango cha elimu ambacho kipo chini.

"Haiwezekani shule iwe na wanafunzi 13 halafu baadhi yao wafeli mtihani hivyo ni vyema wadau wa elimu kuja na mkakati wa ubunifu kuhakikisha kiwango cha elimu kinaongezeka," alisema Mtaka.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Said Sambala, alisema malumbano ya kila siku yamekuwa kero kubwa katika halmashauri hiyo.

Naye Mbunge wa Chemba, Mohammed Moni, alikiri baadhi ya watumishi wa halmashauri hiyo kuwa kikwazo na kupuuza ushauri unaotolewa na viongozi.



# Serikali yaagiza maeneo shule za msingi, sekondari kupewa hatimiliki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeagiza maeneo yote ya shule za msingi na sekondari kupatiwa hatimiliki ili kuepusha uvamizi wa maeneo hayo unaofanywa na baadhi ya wananchi kwa kuanzisha makazi na kufanya shughuli zingine.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, wakati wa kikao cha wadau wa elimu kujadili mambo mbalimbali kuhusu sekta hiyo ikiwamo hali ya ufaulu wa wanafunzi kwenye mitihani ya kitaifa.

Homera aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri zote za mkoa huo kusimamia zoezi hilo na kuhakikisha shule pamoja na majengo mbalimbali ya taasisi za umma yanakuwa na hatimiliki.

Alisema kitendo cha taasisi hizo kutokuwa na hatimiliki kinasababisha migogoro baina ya wananchi na taasisi hizo na kwamba kuna hatari baadhi ya taasisi hizo zikaporwa na watu wasiokuwa na nia njema.

"Jana nilipita pale Shule ya Sekondari Loleza ambayo ni miongoni mwa shule kongwe hapa Mbeya, lakini haina hati, sasa mtu anaweza akafuatilia akapata hati na siku akisema ni mali yake mgogoro utakuwa mzito kwa sababu ana nyaraka na nyie hamna," alisema Homera. Vilevile aliwataka wakurugenzi hao kutembelea mara kwa mara taasisi hizo ili kujiridhisha kama hazivamiwi na wananchi ili kudhibiti uvamizi huo kabla haujaleta madhara.

Akitoa taarifa ya kikao hicho, Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Ernest Hinju alisema lengo la kikao hicho ilikuwa ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya elimu katika kipindi cha mwaka 2021/2022 na kujipanga kwa ajili ya 2022/2023.

Alisema katika kikao hicho walikubaliana kila mdau apambane kuhakikisha eneo analosimamia linafanya vizuri na kwamba haitakiwi wadau hao kuingiliana kwenye majukumu.

Alisema mwaka huu Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo imetekeleza miradi ya elimu vizuri na vyumba vya madarasa viliandaliwa na kukamilika kwa wakati hali iliyosababisha wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kuanza mapema.

Alisema kwa sasa hakuna upungufu wa miundombinu ya shule kama ilivyokuwa inatokea kila mwaka na baadhi ya wanafunzi walikuwa wanachelewa kuanza wakisubiri vyumba vikamilike.

"Fedha za UVIKO-19 zimesaidia sana kukamilisha vyumba vya madarasa na kwa bahati nzuri katika mkoa wetu tulisimamia vizuri sana, sasa ni jukumu letu sisi wadau kuhakikisha tunajipanga kusimamia kila mmoja kwenye kipande chake," alisema Hinju.

Baadhi ya wadau walishauri kuanzishwa kwa utaratibu wa kuboresha shule shikizi kwa ajili ya kukabiliana na mazingira magumu ya elimu hasa maeneo ya vijijini ambako shule zinakuwa mbali na makazi ya watu.



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), Edna Mwaigomole (kushoto), akimkabidhi baadhi ya nyaraka Meneja wa Mamlaka ya Maji Vijijini (RUWASA), Charles Pambe, za miradi miwili iliyotekelezwa na mamlaka hiyo kwa ajili ya miji ya Mlowo na Vwawa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Songwe yakabidhiwa miradi ya maji ya bil. 2.9/-

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya-WSSA), imeikabidhi Mamlaka ya Maji Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Songwe miradi miwili ya maji yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 2.9 ili iendelee kuiendesha kwa kuwahudumia wananchi.

Makabidhiano ya miradi hiyo yalifanyika mwishoni mwa wiki katika Mji wa Vwawa mkoani Songwe ambapo mradi wa kwanza utahudumia wananchi wa Vwawa na mwingine utahudumia wananchi wa Mji wa Mlowo.

Akikabidhi mradi huo kwa uongozi wa RUWASA Mkoa wa Songwe, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mbeya-WSSA, Edna Mwaigomole, alisema miradi hiyo yote imekamilika kwa asilimia 100 na iko tayari kuanza kutumika.

Alisema fedha zilizotumika kujenga miradi hiyo zilitolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya kuboresha huduma za maji kwa wananchi na kuwataka watumiaji wa miradi hiyo kuzingatia sheria ili iwe na faida kwa wananchi.

"Nawashukuru watendaji wote wa Mbeya-WSSA na wa RUWASA Mkoa wa Songwe kwa ushirikiano mliouonyesha wakati wa utekelezaji wa miradi hii, nawaombeni mwendelee na ushirikiano huo," alisema Mwaigomole.

Akipokea miradi hiyo kwa niaba ya serikali, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, alipiga marufuku wananchi kufanya shughuli za kijamii kwenye maeneo ya vyanzo vya maji pamoja na maeneo ya hifadhi za mito.

Alisema shughuli hizo zinaharibu vyanzo na kuchafua maji ambayo yanatumiwa na binadamu na kusisitiza kuwa hatua kali zitaanza kuchukuliwa dhidi ya watakaokaidi katazo hilo.

Alisema uchafuzi wa vyanzo vya maji unasababisha gharama ya kutibu maji hayo kuwa kubwa na hata kuhatarisha afya za watumiaji hasa uchafuzi unaofanywa na shughuli za kilimo ambao unasababisha udongo kujaa kwenye vyanzo.

"Nimeshuhudia mwenyewe hali ya uharibifu wa mazingira kule kwenye vyanzo, lakini nimeona uchafuzi wa maji ulivyofanyika kwenye chanzo chetu, maji yamekuwa mekundu sana kutokana na udongo unaoletwa na maji ya mvua," alisema Mgumba na kuongeza.

"Kilimo chetu watu wa mbozi na mkoa wa Songwe kwa ujumla tunatumia sana mbolea na kemikali zingine, sasa mvua ikinyesha inakusanya na kuleta kwenye maji hali ambayo inahatarisha afya zetu," aliongeza.

Hata hivyo aliagiza watendaji wa kata na vijiji kushirikiana na mamlaka za maji kuainisha maeneo ya vyanzo vya maji na kwenye hifadhi za mito pamoja na kutoa elimu kwa wananchi ili wasifanye shughuli zozote kwenye maeneo hayo.

Baadhi ya wananchi wa mji wa Vwawa waliishukuru serikali kwa kutekeleza miradi hiyo ambayo itawasaidia kupunguza tatizo la upatikanaji wa maji katika mji huo.

Mmoja wa wananchi hao, Rehema Mwashiuya, alisema wamekuwa wakihangaika kutafuta huduma hiyo maeneo ya mbali na makazi yao, lakini kwa sasa huduma hiyo itasogea jirani.

Alisema wanawake ndiyo wanapata shida zaidi ya kutumia muda mwingi kutafuta huduma hiyo badala ya kufanya shughuli za kujiletea kipato.

# Watakiwa kutoa elimu ya lishe kwa jamii

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

WENYEVITI wa mitaa katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa ulioko wilayani Mbarali mkoani Mbeya wametakiwa kuendelea kutoa elimu ya lishe kwa jamii inayowazunguka ili kupunguza matatizo ya utapiamlo na udumavu.

Aidha, wametakiwa kuihimiza jamii kuachana na imani za kishirikina zinazosababisha wananchi kukimbilia kwa waganga wa kienyeji pale watoto wanapoonekana kuwa na dalili za utapiamlo na udumavu wakiamini wamerogwa.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Mbarali, Dk. Izack Kyando, aliyasema hayo kwenye kikao cha Baraza la Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa kilichofanyika mwishoni mwa wiki.

Alisema kumekuwapo na tatizo la baadhi ya wazazi wa kijijini wilayani humo kuwachelewesha watoto kwenda kupata matibabu kwenye vituo vya huduma za afya na badala yake wanakimbilia kwenye tiba za asili wakiamini watoto wao wamerogwa.

Alisema baada ya matibabu hayo ya asili kushindikana ndipo wazazi hao huamua kwenda hospitalini hatua inayohatarisha zaidi maisha ya watoto wao kwa kuwa wengi wanafika wakiwa wamedhoofika.

"Tuwahimize watu kukimbilia hospitali wanapoona watoto wana dalili za udumavu au utapiamlo na si kuendelea kuamini matatizo hayo ni kutokana na imani za kishirikina, mtoto ana dalili za utapiamlo anapelekwa kwa mganga wa jadi hii siyo sahihi kabisa," alisema Dk. Kyando.

Alisisitiza umuhimu wa wajawazito kuhudhuria kliniki akisema pamoja na kumlinda mwanamke ndiyo mwanzo mzuri wa kumkinga mtoto atakayezaliwa kwa kuwa huko zitapatikana taarifa sahihi za maisha yake tangu akiwa tumboni.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rujewa, Chameta Godigodi, aliwataka wenyeviti wa mitaa kuzingatia maagizo hayo ili waendelee kuwa viongozi wanahitaji kuwa na wananchi walio na afya njema.

Aliwasihi wenyeviti hao kutambua kuwa wao ndiyo kioo cha jamii wanayoiongoza ni muhimu wakawa mstari wa mbele kwenye kuhamasisha masuala ya msingi ikiwamo lishe bora, chanjo kwa watoto na pia wajawazito kuhudhuria kliniki.



## ‘Wanafunzi waliorejea kwa utoro watendewe haki’

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima, Mashavu Ahmada Fakih, amewataka walimu wakuu wa shule zenye madarasa ya wanafunzi waliorejea shule baada ya kutoroka kuwashughulikia wanafunzi hao kama walivyo wanafunzi wengine. Alisema kumekuwapo malalamiko kwa walimu wanafundisha wanafunzi hao kutopewa ushirikiano kwa kutengwa na baadhi ya walimu wakuu wao hali inayowapa ugumu katika kuendelea na kazi yao.

Akizungumza wakati alipofanya ziara ya kuwapa wanafunzi hao vifaa vya kusomea kwa baadhi ya wanafunzi wa shule za mkoa wa Kaskazini ‘A’ Unguja, alisema ni vyema kuwapa ushirikiano wa kutosha walimu hao kwasababu wamekuwa wakijitolea kuwaweka vizuri wanafunzi hao.

Mashavu aliwataka wanafunzi hao kusoma kwa bidii na kutotoroka tena shule ili wawe raia wazuri na viongozi bora wa baadaye.

Alisema ni jambo zuri na la faraja kwa wanafunzi hao kuamua kurejea shule kupata haki yao ya elimu kikatiba na ndiyo maana serikali yao kupitia wafadhili mbalimbali imeamua kuwagharamia wanafunzi hao kwa kuwapatia vifaa hivyo ili nao wasome katika mazingira mazuri na salama.

Hata hivyo, aliwaomba wazazi kuendelea kutoa ushirikiano kwa walimu ili kuhakikisha watoto hao hawatoroki tena na wanapata elimu kama lengo la serikali lililokusudiwa.

Kwa upande wao wanafunzi hao wametumia nafasi hiyo kwa kula kiapo cha kutotoroka tena na kuahidi kusoma ili wawe viongozi wazuri wa baadaye na kuzisaidia familia zao.

Vifaa vilivyotolewa ni pamoja na mikoba, sare za shule, viatu pamoja na kampasi, jumla ya shule 22 zimeshapatiwa vifaa hivyo kwa Mkoa wa Kaskazini ‘A’ Unguja kupitia mradi wa kuwarejesha watoto shule, chini ya ufadhili wa Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF).

# Rais Samia azitaka asasi za kiraia ujenzi wa demokrasia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema yupo tayari kufanya kazi na asasi za kiraia katika ujenzi wa taifa, huku akizitaka kuweka mbele maslahi ya taifa na uzalendo katika ujenzi wa demokrasia.

Aliyasema hayo katika hotuba yake iliyosomwa jana kwa niaba yake na Waziri wa Katiba na Sheria, George Simbachawene mjini Unguja wakati akifunga kongamano la asasi za kiraia.

Alisema mchango wa asasi za kiraia umeonekana wazi katika ujenzi wa huduma za jamii, maendeleo na demokrasia ya ushirikishwaji wa wananchi na makundi mengine.

Alisema mafanikio hayo yanahitaji kuendelezwa kwa ushirikishwaji mpana wa makundi mbalimbali yanayounda asasi hizo katika ujenzi wa taifa.

Alisema asasi za kiraia zitapata mafanikio makubwa kama zitaweka uwazi wa shughuli zao katika ufadhili wa miradi na matumizi ya fedha na kuwa na nia njema.

“Hayo ndiyo mambo muhimu ya msingi yataziwezesha asasi za kiraia kusimama na kufanya majukumu yao vizuri kwa masilahi ya walengwa...msikubali asasi za kiraia kutumiwa kwa malengo yenye nia mbaya,” alisema.

Alizitaka asasi za kiraia kutekeleza majukumu yao kwa kufuata sheria pamoja na kuzingatia misingi ya katiba na utawala bora.

Alisema asasi zote zilizoko nchini zimepata usajili kwa mujibu wa malengo yao na amezitaka kufanya kazi vizuri ili malengo hayo yatimizwe.

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na asasi hizo kwa kuzijengea uwezo kuona zinatimiza malengo ya kuanzishwa kwake kwa mujibu wa sheria.

Naye Mwenyekiti wa asasi za kiraia, Haasan Khamis Juma, aliwasilisha mapendekezo sita yenye lengo la kujenga uhusiano mzuri kati ya serikali na asasi hizo katika utekelezaji wa majukumu yao.

Baadhi ya mapendekezo hayo ni kushirikishwa kikamilifu katika utendaji wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kupata taarifa za serikali ya utekelezaji wa majukumu muhimu.



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (kulia), akipokea zawadi kutoka visiwa vya Unguja na Pemba kwa Katibu wa Habari na Uenezi wa tawi la Mchangani wa chama hicho, Farahani Mohammed Msuri, aliyopewa na wananchi wa Jimbo la Malindi Mjini Unguja alipotembelea jimbo hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madalali waonywa kunadi samaki wachanga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao Baharini Zanzibar, Dk. Salum Sudi Hammed, amewataka madalali wa mnada kuacha tabia ya kunadi samaki wachanga wanaoletwa sokoni na baadhi ya wavuvi jambo ambalo ni kosa kisheria.

Dk. Salum alisema hayo mjini hapa baada ya kukutana na kamati za uvuvi, masheha na kamati ya soko katika utoaji wa elimu ya umuhimu wa takwimu, ukataji wa leseni pamoja na ukaaji wa diko kwa wavuvi.

Dk. Salumu alisema hakuna budi kufuata sheria ya uvuvi na kusimamia rasilimali za bahari kutokana na kukithiri kwa uvuvi haramu unaoharibu mazingira ya bahari pamoja na wavuvi wasiokata leseni za kuvulia jambo linalorudisha nyuma juhudi za serikali.

Dk. Salum alisema kuna umuhimu kwa wavuvi kukaa nao kwa kufuata taratibu maalumu zilizowekwa na serikali kwa ajili ya maendeleo ya taifa nchini na kwenda sambamba na dhana ya uchumi wa buluu.

Aliwataka wavuvi kutoa ushirikiano kwa taasisi za serikali kushiriki zoezi la kuhesabiwa wakati wa sensa ya wavuvi nchini kwa lengo la kufanyiwa makubwa zaidi na serikali.

“Wavuvi wote mnatakiwa kukubali kuhesabiwa hivyo muanze kuelimishana ili kulipa zoezi la sensa ya wavuvi kufanyika kwa uhakika bila ya kuachwa mvuvi yeyote yule,” Dk. Salum alisema.

Naye Ofisa uvuvi wa kienyeji, Mwanahamis Mohammed Ali, kutoka Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, alisema Idara inajukumu la kutoa leseni za uvuvi pamoja na kusajili chombo cha kuvulia kwa lengo la kukuza pato la serikali na kutambulika mvuvi kisheria yanapotokea maafa.

“Idara inatoa leseni za uvuvi, leseni za chombo pamoja na leseni za kusafirishia mazao ya baharini kupitia sheria ya mwaka 2010 imekataza mvuvi kuvua samaki bila ya leseni ya chombo na kuvulia,” alisema.

Kwa upande wake, Ofisa wa ufuatiliaji na tasmini, Daud Haji Pandu, kutoka Idara ya Uvuvi Zanzibar, alisema changamoto ya wavuvi wa dago kutakiwa kukata leseni Tanzania Bara inatokana na kukwepa kukata kibali cha ruhusa pamoja na ya kuvulia jambo ambalo ni ukiukwaji wa taratibu za kwenda dago kisheria kwa wilaya yoyote ile ya nchini Tanzania Bara na Zanzibar.

“Utaratibu wa kwenda dago mvuvi anatakiwa kuchukua barua kwa sheha wa shehia anayotoka kwa ajili ya kuombewa ruhusa ya kupatiwa kibali maalumu cha kukaa dago kisheria katika wilaya atayokwenda kufanya shughuli za uvuvi,” alisema Daud.

Akizungumza kwa niaba ya sheha wa shehia ya Kiembe Samaki Othman Talib, aliiomba idara husika kuwawekea muundo mmoja wa usimamizi wa kamati ya uvuvi na kamati ya soko kushiriki pamoja shughuli zote za kiutendaji.

Mwenyekiti wa kamati ya uvuvi, Nachia Abdull Mwinyi, ameiomba serikali kuwasaidia kupata umiliki wa waraka katika eneo la Soko la Mazizini kwa urahisi ili kuondoa migogoro ya hapa na pale inayojitokeza.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA

PROBATE AND ADMINISTRATION
CASE NO. 205/ 2021

IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE MERINA FUNGO CHIPALO of IYUMBU Area within Dodoma Region.
AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ANNASTAZIA JOHN CHIPALO

**GENERAL CITATION**
(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **18 Day of MARCH, 2022**
**Date at Dodoma this 20TH day of December,2021.**

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CLEMENCIA BERNARD KIZUGHUTO**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya GARI(raum) yenye namba za usajili **T 501 DFX** yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0782066296**

**DSM /PHQ/RB/100115/2022**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMMANUELY EZEKIA MGAYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI CANTER** yenye namba za usajili **T 553 CRR,** Chassis no **FE648E522187,** Engine NO **4D378451256,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa

**MKB/RB/22/2022**

---

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO

DISTRICT AT MOROGORO

PROBATE AND ADMINISTRATION

CAUSE NO 29 OF 2022

In the Matter of the Estate of the Late TABU ALLY MKOPI

By 1GRACE ALOYCE MVULA.
2. ......................................

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 15day of 03 ..2022

Dated at Morogoro this 28 day of 02 ..2022

RESIDENT MAGISTRATE

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KUITWA SHAURINI MDAIWA
[MCA/63]

MAHAKAMA YA MWANZO MTIBWA
WILAYA YA MVOMERO

MADAI NAMBARI 4 2022

**Mdai** ..................................................**JAMHURI SEFU MNGUBILI**

**ANAMDAI**

**Mdaiwa**............................................ **JUMA ZUBERI MSUKULU**

**Kwa JUMA ZUBERI MSUKULU**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba/ eleza hapa habari za madai:-
**TALAKA**
Kwa hiyo unahitajiwa/ mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya ALHAMIS tarehe 24/03/2022 saa 2:00 asubuhi kwa kujibu madai hayo, na kwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu unahati zote zinazihusu shauri hilo kwaajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu . Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 10-03-2022

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo

---

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO

DISTRICT AT MOROGORO

PROBATE AND ADMINISTRATION

CAUSE NO 31 OF 2022

In the Matter of the Estate of the Late EMERENSIANA PETER STEPHAN

By 1.MARIA PETER STEPHAN
2. ......................................

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 17 day of 03…2022

Dated at Morogoro this 03 day of 03…2022

RESIDENT MAGISTRATE

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO……… 2022

IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE HILDA ZAKARIA MSOGA of MSALATO within Dodoma Region.

AND

IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY STANLEY ZAKARIA MSOGA

**GENERAL CITATION**
(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 16 Day of 03, 2022

Date at Dodoma this 24TH day of January,2022.

RESIDENT MAGISTRATE

---

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 23/ 2022

IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE EGLA OBED MAMOTTO of MAKOLE within Dodoma Region.

AND

IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY THOMAS LUCAS HOYA

GENERAL CITATION
(RULE 75 PROBATE RULES GN369 OF 163)

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 16 Day of 03, 2022

Date at Dodoma this 20TH day of January, 2022

RESIDENT MAGISTRATE

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**VERONICA KISHA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P.0660/0209** kilichotolewa na shule/kituo cha **MOROGORO TEACHER'S COLLEGE** mwaka 2017, yeyote atakayekiokota ataoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/URA/RB/104984/2022**

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

---

## FANIKIWA MICROFINANCE LIMITED

### TANGAZO LA MNADA

**WORK ETHIC COMPANY LIMITED** Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Magari na Nyumba katika jiji la Dar es salaam ,Wadaiwa wanashauriwa kulipa madeni yao ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe za Mnada Zinavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | Mahali dhamana ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Benezeth Kyaruzi Benedict | Gari- MAZDA BONGO T221DJY,Mikocheni | 30.03.2022 |
| Cuthbert Boniface Fungo | Gari-TOYOTA HARRIER T670DNA,Mikocheni | 30.03.2022 |
| Jerome Geofrey Mremi | Gari-TOYOTA RUNX T690DTX,Mikocheni | 30.03.2022 |
| Shabani Omary Kibwana | Nyumba ipo Pugu –Dar es salaam | 31.03.2022 |

**Masharti ya Mnada.**
1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25%(au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%)litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa Mawasiliano piga 0623662447,0677014355, au 0717956315.**

116748902

---

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

SIKU YA 20;

# Mashambulizi ya Russia Ukraine

• Russia yakanusha kuomba msaada wa kijeshi China



Kikosi cha Zimamoto kikimsaidia mkimbizi nchini Ukraine kuelekea nchi jirani kwenye mpaka wa Romania -Ukraine, eneo la Siret, jana. **PICHA: AP**

**Kyiv,** UKRAINE

RUSSIA imesema kwamba haijaomba msaada wa vifaa vya kijeshi kutoka China, ikisema inajitosheleza yenyewe.

Ikiwa ni siku 20 tangu Russia ianze mashambulizi ya kijeshi Ukraine, Inakadiriwa takribani wakimbizi kutoka Ukraine wanafikia milioni 2.6 huku wengi wao wakiwa watoto na wanawake.

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy kwenye hotuba yake kupitia televisheni, amesema serikali yake imeamua kupunguza makali ya ushuru na kodi kwa biashara ndogo kutokana na haki iliyoko nchini mwake kwa sasa.

Wakati rais huyo akitangaza hayo, pia siku ya jana ilikuwa ni awamu ya nne ya mazungumzo kati ya nchi hizo, ingawa awamu za wali hazikuzaa matunda.

"Mazungumzo kati ya Russia na Ukraine yameanza ingawa mawasiliano ya pande mbili yamekuwa ni magumu," Mshauri wa Rais wa Ukraine, Mykhailo Podolyak amesema hayo kwenye ukurasa wake Twitter.

Msemaji wa Kremlin Dmitry Peskov, akizungumza kuhusu Russia kuomba msaada wa kijeshi, kwa mujibu wa taarifa kutoka Marekani, amesema taarifa hizi si za kweli, na kwamba nchi yake imejitosheleza.

Kulingana na gazeti la New York Times, lilidai kwamba Russia, imeomba usaidizi wa kiuchumi na kijeshi kutoka China ili kuendesha vita na kukwepa vikwazo vya Magharibi.

Mshauri wa masuala ya usalama wa Marekani Jake Sullivan ameionya Beijing kwamba kutakuwa na madhara kwa kuisaidia Magharibi.

**Mkuu wa Polisi wa Kyiv, Andriy Nebytov, amedai kuwa mwandishi huyo alilengwa na wanajeshi wa Russia na kwamba waandishi wengine wawili walijeruhiwa na kupelekwa hospitali.**

Wakati hayo yakiendelea, wapatanishi wa Russia na Ukraine wameanza duru ya nne ya mazungumzo yenye lengo la kusitisha mzozo. Mpatanishi wa Ukraine Mykhailo Podolyak amesema mazungumzo hayo yatalenga kuweka usitishaji vita, kuondolewa kwa wanajeshi wa Russia na kudhamini usalama wa Ukraine.

Licha ya matarajio hayo, mashambulizi ya Urusi yameendelea huku majeshi yake yakishambulia jengo la ghorofa na kiwanda cha kutengeneza ndege katika mji mkuu, Kyiv.

Aidha, Ukraine imeendelea kuwahamisha raia walionaswa kupitia maeneo 10 ya misaada kiutu, ikiwa ni pamoja na kuwatoa miji iliyo karibu na Kyiv na eneo la Mashariki la Luhansk.

Shirika la habari la Reuters liniripoti kwamba India inafikiria kuchukua ofa ya Russia ya kununua mafuta ghafi na bidhaa zake nyingine kwa bei iliyopunguzwa, huku kukiwa na vikwazo vikali vya Magharibi dhidi ya Moscow.

### MWANDISHI AUAWA

Kwa mara ya kwanza tangu Februari 24, mwaka huu, Russia ilipoivamia Ukraine kijeshi, jana imeripotiwa kifo cha mwandishi wa habari wa Marekani anayefanya kazi nchini Ukraine, kuuawa akiwa kwenye majukumu ya kazi.

Taarifa zinasema ameuawa kwa kupigwa risasi katika mji wa Irpin, nje ya Kyiv.

Brent Renaud, mwenye umri wa miaka 50, alikuwa mwandishi wa habari na mtengenezaji wa filamu ambaye alikuwa akifanya kazi katika eneo hilo kwa muda mrefu.

Mkuu wa Polisi wa Kyiv, Andriy Nebytov, amedai kuwa mwandishi huyo alilengwa na wanajeshi wa Russia na kwamba waandishi wengine wawili walijeruhiwa na kupelekwa hospitali.

Hicho ni kifo cha kwanza kuripotiwa cha mwandishi wa habari wa kigeni anayeripoti vita nchini Ukraine.

Mmoja wa waandishi wa habari aliyejeruhiwa, Juan Arredondo, alimwambia mwandishi wa habari wa Italia kwamba, alikuwa pamoja na Renaud wakati waliposhambuliwa.

"Tulikuwa kwenye moja ya madaraja huko Irpin, tukienda kupiga picha za wakimbizi waliokuwa wanaondoka, na tukaingia kwenye gari," anasema katika video iliyochapishwa kwenye Twitter.

"Kuna mtu alijitolea kutupeleka kwenye daraja lingine na tulivuka kituo cha ukaguzi, kabla ya kuanza kutufyatulia risasi. Kwa hivyo dereva akageuza, waliendelea kupiga risasi; tulikuwa sisi wawili. Rafiki yangu Brent Renaud, akapigwa risasi ... nilishuhudia akipigwa risasi shingoni," anasema.

### RUSSIA YAIKARIBIA KYIV

Wanajeshi wa Russia wameendeleza harakati zao za kijeshi kuelekea mji mkuu wa Ukraine, mapigano yameendelea viungani mwa Kyiv.

Maofisa wa Ukraine wamesema wanajeshi wa Russia walifyatua makombora nje ya mji huo mkuu ambapo raia wawili wameuawa.

Rais Zelensky ameitaka Jumuiya ya Kujihami Nchi za Magharibi (NATO), kutangaza amri ya kutoruka ndege katika anga yake.

Mshauri wa Rais wa Ukraine Mykhailo Podolyak amesema maofisa wa Ukraine na Russia wanakutana tena leo kujadili miongoni mwa masuala mengine, upelekaji wa chakula, maji na dawa pamoja na bidhaa nyingine katika miji na vijiji vinavyokabiliwa na mashambulizi.

### MSAADA NISHATI MBADALA

Kampuni ya kibiashara ya Uingereza kupitia katibu wa Kwasi Kwarteng imesema imetoka msaada wa majenereta takribani 500 kuisaidia kwa ajili ya majengo 20,000 nchini Ukraine kuondokana na vikwazo vya nishati baada ya Russia kuathiri mfumo wa umeme katika baadhi ya vyanzo vikuu ikiwamo cha nyuklia.

**Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao**

HABARI MICHEZO

# MSUVA AIPA TANO SIMBA CAF, AITABIRIA MAKUBWA

Adam Fungamwango na Saada Akida

WINGA wa Klabu ya Wydad Casablanca ya Morocco na Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Simon Msuva, ameipongeza Timu ya Simba kwa kushinda mechi yake ya Kombe la Shirikisho Afrika (CAF), dhidi ya RS Berkane ya nchini humo, akishauri kuwa imefika wakati sasa kuanza kuangalia kushinda ugenini pia.

Msuva, ambaye kwa sasa ana mgogoro na timu yake hiyo na kumfanya awepo hapa nchini, alikuwa mmoja wa mashuhuda wa mechi hiyo juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Simba ikishinda bao 1-0, alisema Simba ina timu nzuri na wachezaji wake ni wa viwango vya juu, ila wanatakiwa kuzidisha juhudi kwa sababu wanaiwakilisha nchi kwa sasa.

"Hawa RS Berkane si wabaya, nadhani hali ya hewa imewaathiri, unajua kwa sasa nchini Morocco kuna baridi sana na mechi zao huwa zinachezwa usiku kwa hiyo kucheza mchana jua kali kumewasumbua sana.

Kingine ni kwamba Simba ilikuwa nyumbani, na ni kawaida yao kuutumia vizuri uwanja huo, si wageni pia kwenye michuano hii, kwa sasa wana uzoefu mkubwa kwa sababu ya kucheza mara kwa mara, ila nawashauri wasifanye hivi nyumbani tu, waanze sasa kuanza kushinda na ugenini itawasaidia sana," alisema winga huyo wa zamani wa Yanga.

Naye mchezaji wa Simba Clatous Chama amebainisha kuwa mara nyingi timu za Afrika Kaskazini, maarufu kama timu za Waarabu hufanya kashikashi kwa lengo la kuwatisha waamuzi, hasa wanapoona hali inakuwa mbaya kwao.

**"Tumepata kitu ambacho tulichokuwa tunakitafuta na mpaka sasa kundi lipo wazi, hadi mwisho,ndiyo tutajua tupo wapi, lakini naamini tutavuka tu hili kundi.**

Wale walianza kulalamika tangu mwanzo, Waarabu wako hivi, kwa sababu huwa na tabia ya kumtisha mwamuzi, hili liwe fundisho hata kwetu,

wao kitu kidogo tu wanalalamika sana, hata sisi huwa tunafanyiwa mambo mengi kwao, lakini huwa hatulalamiki," alisema Chama. Baada ya ushindi huo, Simba inaongoza Kundi D, ikiwa na pointi saba, ikifuatiwa na Asec Mimosas ya Ivory Coast ambayo juzi iliichapa US Gendamarie ya Niger, ikiwa na pointi sita sawa na RS Berkane iliyoko nafasi ya tatu ikiwa, huku US Gandamarie ikiburuza mkia na zake pointi nne.

WAYAAA...




Kiungo wa Arsenal, Mghana Thomas Partey (jezi nyekundu), akiifungia timu yake bao la kwanza kwa kichwa wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Leicester City kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi. **PICHA: MTANDAO**

## Mkandala asakwa, kung'olewa Dodoma Jiji

Na Adam Fungamwango

BAADA ya kuonyesha uwezo mkubwa kwenye mechi dhidi ya Simba, kuna taarifa kuwa klabu kadhaa zimeanza kumsaka kiungo mshambuliaji wa Dodoma Jiji, Cleophace Mkandala, wakati huu akiwa amebakisha miezi mitatu tu kumaliza mkataba wake na klabu hiyo.

Mkandala aliyewafunika kabisa viungo wa Simba na kuwachachafya mabeki wake kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyochezwa Machi 7, mwaka huu, inadaiwa baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, klabu mbalimbali ikiwamo Simba yenyewe imeanza mazungumzo naye.

Hata hivyo, Meneja wa Mchezaji huyo, Kelvin Frednand, amesema mpaka sasa hajapokea ofa yoyote si kutoka nje ya nchi na klabu za ndani tu, bali hata na Dodoma Jiji wenyewe.

"Alisaini mkataba wa miaka miwili, alitumikia mmoja na sasa anamalizia, amebakisha miezi mitatu na hatujapata ofa yoyote kutoka nje ya nchi, ndani ya nchi hata klabu yake ya Dodoma Jiji bado haijakaa na sisi kuangalia kama wanaweza kuongeza mkataba, lakini sisi wenyewe tumeona kwanza aendelee kucheza mpaka mkataba utakapoisha.

"Baada ya hapo ndiyo tutajua kama atasalia Dodoma Jiji, atapata timu ndani ya nchi, au nje ya nchini ambako yeye mwenyewe anapenda kwenda kwa sababu hakutokuwa na pesha kama timu za hapa nchini," alisema meneja huyo.

Alisema uwezo anaoendelea kuonyesha unaweza kumfanya awe na gharama kubwa ligi ikishamalizika, hivyo kwa sasa wameamua kuacha amalizie ligi kwanza.

"Haujafika muda wa kutoa jibu sahihi, ukifika tutatoa." alisema.

Tetesi zinadai kwamba baada ya mechi hiyo kumalizika, kuna baadhi ya viongozi wa Simba walionekana kuvutiwa naye na kuonyesha nia ya kutaka kuwa naye kwa msimu ujao, huku pia Yanga, Azam, KMC na Namungo zikionyesha kuvutiwa na mchezaji huyo, ambaye kabla ya hapo alichezea Tanzania Prisons.

## Mbeya Kwanza FC: Hatutashuka daraja

Na Adam Fungamwango

PAMOJA na kuchapwa mabao 2-0 juzi kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma dhidi ya Dodoma Jiji FC, timu ya Mbeya Kwanza imedai kuwa haitoshuka daraja na watapigana hadi tone la damu la mwisho.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mwaka Mwalwisi, amesema kuwa wameanza kujipanga kutumia vema uwanja wa sasa wa nyumbani, Majimaji Songea ilikohamia kwenye mechi za mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, ili kuhakikisha inapata ushindi na timu inasalia kwenye Ligi Kuu.

"Timu yetu si mbaya, tunaweza kucheza na yoyote ile, kama mlivyoona tulicheza na timu kubwa, lakini tukatoa ushindani mkubwa sana, tunarudi kwenye uwanja wetu, tutahakikisha tunatumia vizuri uwanja wetu wa sasa wa Majimaji Songea kupata ushindi kuhakikisha hatushuki," alisema kocha huyo.

Naye Meneja wa timu hiyo, David Naftari, amesema kupoteza mechi zao na kukaa sehemu mbaya kwenye msimamo wa ligi ni upepo mbaya tu wanaopitia na si kwamba kuna madai ya wachezaji ndani ya klabu.

"Hakuna mchezaji anayedai mshahara wala posho, klabu haidaiwi na uongozi upo kamili, huu ni upepo mbaya tu umetupitia. Na si sisi tu, zipo timu hata kubwa zimepitia kwenye changamoto kama hii yetu, na hata huko chini hatupo peke yetu, hata Prisons, Mtibwa Sugar zipo chini, lakini tutahakikisha tunapambana kwa mechi zilizobaki ili kuepuke kukaa kwenye nafasi mbaya," alisema Naftari.

Mbeya Kwanza ipo nafasi ya 15 kati ya timu 16 zinazoshiriki Ligi Kuu, ikiwa ina pointi 14 tu kwa mechi 18 ilizocheza.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ARSENAL KWA COUTINHO
KLABU ya Aston Villa ina kipengele cha kumnunua, Philippe Coutinho, lakini Arsenal inamtaka nyota huyo mwenye miaka 29 kutoka Barcelona msimu huu wa majira ya joto kama hatajiunga moja kwa moja katika kikosi hicho cha Steven Gerrard. (***Sport***)

### ZIDANE ANUKIA PSG
ZINEDINE Zidane anatajwa huenda akamrithi Mauricio Pochettino kama kocha wa PSG na tayari ameanza kuangalia nyota wa kuwasajili kutoka klabu yake ya zamani ya Real Madrid, akiwamo kiungo Mbrazil Casemiro mwenye umri wa miaka 30. (***El Nacional***)

### HAALAND KWENDA HISPANIA
KIPAUMBELE cha Erling Braut Haaland katika dirisha la majira ya joto ni kuelekea Hispania kujiunga na Real Madrid au Barcelona, licha ya ripoti za mwishoni mwa wiki kudai kwamba mshambuliaji huyo Mnorway wa Borussia Dortmund mwenye umri wa miaka 21, amekubali mpango wa kujiunga na Manchester City. (***Sport***)

### TRAORE KUBAKI BARCA
BARCELONA wanataka kumsajili moja kwa moja winga wà Hispania anayecheza klabuni hapo kwa mkopo akitokea Wolves , Adama Traore mwenye umri wa miaka 26, na wapo tayari kukamilisha dili hilo katika dirisha la majira ya joto huku wakiwa tayari kumtoa kiungo wa Hispania, Riqui Puig mwenye umri wa miaka 22 ili kufanikisha mpango huo. (***90Min***)

### WIRTZ AWANIWA LIVER, UTD
WASAKA vipaji kutoka Manchester United, Liverpool na Newcastle wamekuwa wakimfuatilia nyota wa kimataifa wa Ujerumani anayeichezea Bayer Leverkusen, Florian Wirtz, lakini kiungo huyo mshambuliaji mwenye umri wa miaka 18, amepata majeraha makubwa yatakayomweka nje ya uwanja msimu mzima. (***Express***)

### DI MARIA KUONDOKA PSG
WINGA wa Argentina, Angel di Maria mwenye umri wa miaka 33, ameamua kwamba anataka kuondoka Paris St-Germain msimu huu na anaweza kurejea Benfica. (***AS***)

### POCHETTINO, MBAPPE KUSEPA
KOCHA Mauricio Pochettino na mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23, ni miongoni mwa majina makubwa yatakayoondoka Paris St-Germain msimu huu. (***L'Equipe, via Mirror***)

### VIDAL KWENDA FLAMENGO
ARTURO Vidal mwenye umri wa miaka 34, anajiandaa kutimka Inter Milan msimu huu, huku klabu ya Flamengo ikionyesha nia ya kumrejesha Amerika Kusini kiungo huyo wa Chile. (***Calciomercato***)

### RABIOT KUWEKWA SOKONI
JUVENTUS iko tayari kumuuza kiungo Mfaransa Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 26, msimu huu. (***Calciomercato***)

### LAPORTA NA HAALAND
RAIS wa Barcelona, Joan Laporta anasema klabu hiyo hatamsajili Erling Haaland katika dirisha la majira ya joto kama uhamisho wake utawaweka vigogo hao wa Hispania kwenye hatari ya mgogoro wa kifedha. (***TV3, via Goal***)

### DEST AWANIWA ROMA
AS Roma wanajiandaa kupeleka ofa msimu huu kwa ajili ya mlinzi wa pembeni wa Barcelona raia wa Marekani, Sergino Dest mwenye umri wa miaka 21. (***Corriere dello***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL: SINA MPANGO NA MANCHESTER UNITED

**Kwanza kabisa napenda hapa nilipo, kwa sababu naiona thamani ya mimi kuwa kwenye hii klabu...**

**LONDON,** ENGLAND

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amesisitiza kuwa ana furaha kwenye klabu yake ya sasa ingawa hajui hatima yake kutokana na vikwazo alivyowekewa mmiliki wa klabu hiyo, Roman Abramovich, kutoka kwa Serikali ya Uingereza.

Manchester United mwishoni mwa msimu huu wanatafuta kocha ambaye atachukua majukumu ya kuinoa timu baada ya muda wa Ralf Rangnick kuisha na kuhamia kwenye nafasi yake ya ushauri.

Na United wanataka kutumia nafasi kwa yanayoendelea sasa kwenye klabu ya Chelsea ili kuweza kumchukua Tuchel kuinoa timu hiyo.

Kutokana na wimbi zito linaloikabili klabu hiyo, Tuchel amesisitiza kuwa yeye atabaki hapo kufanya kazi yake na kuhakikisha timu inapata matokeo mazuri uwanjani msimu huu.

**"Kwa yanayoendelea siku hadi siku, hakuna utatuzi kwa kipindi hiki," alisema Tuchel akinukuliwa na BBC Sport.**

"Kwanza kabisa napenda hapa nilipo, kwa sababu naiona thamani ya mimi kuwa kwenye hii klabu na akili yangu iko sawa hapa.

"Kuna thamani napewa hapa na najiona kama mwenye bahati, najua ni kwa kiasi gani nahitaji kuwa bora zaidi. Ni thamani kubwa sana kwangu.

"Sijawahi kuwa na ukomo wa mkataba wa kiwango cha fedha ninachotumia au kiasi cha fedha ambacho nahitaji kwa mchezaji, sijawahi fanya hivi kwenye klabu yoyote.

"Najiamini mwenyewe kuweza kukabiliana na hali yoyote, naamini uwezo wangu wa kuhamasisha timu. Nina furaha kuwa sehemu ya timu hapa Chelsea.

"Nina furaha sana, na natumai haitabadilika."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,042

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
ATLETICO MADRID
1 | 2.26
X | 3.10
2 | 3.39

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MESSI, NEYMAR YAWAKUTA PSG



**PARIS,** Ufaransa

WACHEZAJI wa Paris Saint-Germain, Neymar na Lionel Messi walizomewa kila walipogusa mpira na mashabiki wa klabu hiyo wakati wa mchezo wa Ligue 1 dhidi ya Bordeux, Jumapili baada ya kutolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mashabiki wa PSG walikasirishwa kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Real Madrid katikati ya wiki kwa jumla ya mabao 3-1.

Mashabiki wa PSG wanaona kwamba, Messi na Neymar wameshindwa kuisaidia timu kusonga hatua inayofuata.

Kelele zilianza kusikika pale majina ya Neymar na Messi yalipotangazwa huku seti zote za wachezaji zikiwa zimepangwa kabla ya mchezo kuanza, na kuendelea katika dakika 30 za kwanza.

PSG iibuka na ushindi wa mabao 3-0 katika mchezo huo dhidi ya Bordeux, shukrani kwa Mbappe, Neymar na Parades walioofumania nyavu juzi.



# Xavi ammwagia sifa Torres

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Xavi anasema hana shaka kwamba Ferran Torres angeanza kung'ara akiwa na klabu hiyo baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania kufunga mabao mawili katika ushindi wa 4-0 dhidi ya Osasuna Jumapili.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, alikuwa amefunga bao moja pekee katika mechi sita za Ligi Kuu Hispania, LaLiga, baada ya kuhama kwake kutoka Manchester City, lakini alitikisa nyavu mara mbili katika ushindi wa kawaida uliowapandisha 'Blaugrana' hao hadi nafasi ya tatu kwenye msimamo.

Bao lake la kwanza alifunga kwa mkwaju wa penalti baada ya Gavi kuchezewa vibaya eneo la hatari na akaongeza la pili kwa asisti ya Ousmane Dembele.

Mabao hayo mawili ni ya kwanza katika mechi 78 kwenye LaLiga - yalitokana na mashuti manne pekee, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 akiwa amefunga mara moja tu katika majaribio yake 16 ya awali kwenye Ligi Kuu Hispania.

Xavi alifurahishw na mchango wake alisisitiza kuwa ha shaka kwamba Torr angeng'ara hapo Car Nou hivi karibuni.

"Nikiwa na Ferran yari nilisema kwam mabao yatakuja; lilikuv suala la muda," aliser Xavi akiwaambia waan shi wa habari.

"Mbali na hayo, ka yote na kile anachotu mbele."

Huo ulikuwa ni ushin wa 12 katika michezo iliyopita ya LaLiga, mab mengine mawili yakifur wa na Pierre-Emerick A bameyang na Riqui Puig

## HABARI MICHEZO


# 2,431,860 JACKPOT

## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 19/03/22 | 18:00 | Huddersfield vs Bournemouth | 2.51 | 3.29 | 2.65 |
| 02. 19/03/22 | 18:00 | Reading vs Blackburn | 2.60 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 19/03/22 | 18:15 | Eupen vs Mechelen | 2.76 | 3.40 | 2.39 |
| 04. 19/03/22 | 20:45 | GO Ahead Eagles vs Cambuur | 2.48 | 3.45 | 2.70 |
| 05. 19/03/22 | 23:00 | Nantes vs Lille | 2.87 | 2.97 | 2.63 |
| 06. 20/03/22 | 14:30 | Venezia vs Sampdoria | 2.55 | 3.35 | 2.70 |
| 07. 20/03/22 | 15:30 | Jahn Regensburg vs Paderborn | 2.75 | 3.24 | 2.45 |
| 08. 20/03/22 | 16:00 | Gaziantep BB vs Galatasaray | 2.71 | 3.36 | 2.45 |
| 09. 20/03/22 | 17:00 | Bordeaux vs Montpellier | 2.40 | 3.45 | 2.80 |
| 10. 20/03/22 | 17:00 | Empoli vs Verona | 3.20 | 3.40 | 2.20 |
| 11. 20/03/22 | 18:00 | Ponferradina vs Eibar | 2.50 | 3.09 | 2.80 |
| 12. 20/03/22 | 18:15 | Celta Vigo vs Betis | 2.41 | 3.34 | 2.89 |
| 13. 20/03/22 | 20:00 | Roma vs Lazio | 2.34 | 3.41 | 2.96 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 15/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 5106 | Police FC (UGA) vs Kampala City Council | 5.20 | 3.35 | 1.75 |
| 16:00 | 5732 | Dove All Stars vs Bright Stars | 2.13 | 3.03 | 3.32 |
| 16:15 | 5602 | Al Jabalain vs Jeddah Club | 1.92 | 3.13 | 3.86 |
| 17:00 | 4920 | Real Kashmir vs Neroca FC | 2.19 | 3.13 | 3.09 |
| 18:00 | 3374 | Slovan Bratislava vs Zlate Moravce | 1.08 | 8.50 | 17.38 |
| 20:30 | 1843 | Crotone vs Frosinone | 3.73 | 3.39 | 1.93 |
| 20:30 | 2267 | Cosenza vs Lecce | 4.61 | 3.53 | 1.73 |
| 20:30 | 3979 | Cittadella vs Reggina | 1.92 | 3.23 | 4.01 |
| 20:30 | 4306 | Brescia vs Benevento | 2.17 | 3.14 | 3.33 |
| 20:30 | 4783 | Vicenza vs Parma | 2.65 | 3.23 | 2.55 |
| 20:30 | 5920 | Como vs Ternana | 2.61 | 3.20 | 2.61 |
| 20:45 | 2762 | Legia Warszawa vs Nieciecza KS | 1.52 | 3.93 | 5.37 |
| 21:00 | 2549 | Nimes vs AJ Auxerre | 2.70 | 3.14 | 2.55 |
| 21:00 | 2595 | Nancy vs Paris FC | 3.48 | 3.28 | 2.05 |
| 21:00 | 3954 | Valenciennes vs Caen | 2.51 | 3.15 | 2.75 |
| 21:00 | 4130 | Coca Cola vs Smouha Club | 2.19 | 3.01 | 3.50 |
| 21:00 | 4981 | Toulouse vs Amiens | 1.51 | 3.93 | 6.09 |
| 22:30 | 3891 | Alessandria vs Monza | 3.48 | 3.19 | 2.09 |
| 22:45 | 1149 | Swindon Town vs Sutton United | 2.26 | 3.34 | 2.95 |
| 22:45 | 1268 | Rotherham vs Lincoln | 1.44 | 4.41 | 6.27 |
| 22:45 | 1505 | Stockport vs Notts County | 1.80 | 3.56 | 4.00 |
| 22:45 | 1608 | Tranmere vs Harrogate | 2.21 | 3.29 | 3.09 |
| 22:45 | 1766 | Rochdale vs Salford City | 2.19 | 3.29 | 3.14 |
| 22:45 | 1798 | Hartlepool vs Bradford City | 2.26 | 3.29 | 3.00 |
| 22:45 | 1955 | Exeter vs Crawley Town | 1.74 | 3.58 | 4.41 |
| 22:45 | 2039 | Walsall vs Oldham | 2.02 | 3.39 | 3.44 |
| 22:45 | 2084 | Barnet vs Boreham Wood | 4.20 | 3.71 | 1.73 |
| 22:45 | 2562 | Birmingham vs Middlesbrough | 3.18 | 3.28 | 2.17 |
| 22:45 | 3022 | Plymouth vs Portsmouth | 2.27 | 3.29 | 2.99 |
| 22:45 | 3077 | Crewe vs Wigan | 5.90 | 4.13 | 1.50 |
| 22:45 | 3246 | Charlton vs Gillingham | 1.71 | 3.73 | 4.42 |
| 22:45 | 3434 | Cowdenbeath vs Forfar Athletic | 4.12 | 3.60 | 1.73 |
| 22:45 | 3481 | Bristol Rovers vs Colchester | 2.01 | 3.30 | 3.59 |
| 22:45 | 3489 | Port Vale vs Mansfield | 2.19 | 3.19 | 3.24 |
| 22:45 | 3760 | Crusaders Belfast vs Ballymena Utd | 1.16 | 6.17 | 13.50 |
| 22:45 | 3784 | Wycombe vs Fleetwood Town | 1.65 | 3.83 | 4.71 |
| 22:45 | 3817 | Forest Green vs Leyton Orient | 1.68 | 3.68 | 4.71 |
| 22:45 | 3855 | Carlisle vs Newport | 2.94 | 3.24 | 2.32 |
| 22:45 | 4006 | Halifax vs Bromley | 1.98 | 3.37 | 3.52 |
| 22:45 | 4034 | Stevenage vs Northampton | 2.75 | 3.15 | 2.51 |
| 22:45 | 4714 | Bournemouth vs Reading | 1.34 | 4.90 | 7.64 |
| 22:45 | 4851 | Barnsley vs Bristol City | 2.37 | 3.19 | 2.90 |
| 22:45 | 4927 | Blackburn vs Derby | 1.75 | 3.39 | 4.71 |
| 22:45 | 5282 | Southend vs Dagenham and Redbridge | 2.42 | 3.36 | 2.68 |
| 22:45 | 5499 | Shrewsbury vs Morecambe | 2.02 | 3.10 | 3.83 |
| 22:45 | 5540 | Scunthorpe vs Barrow | 3.13 | 3.38 | 2.15 |
| 22:45 | 5541 | Sheffield Wed vs Accrington | 1.54 | 4.01 | 5.47 |
| 23:00 | 1882 | West Bromwich vs Fulham | 3.43 | 3.38 | 2.03 |
| 23:00 | 3369 | Manchester Utd vs Atletico Madrid | 2.26 | 3.10 | 3.39 |
| 23:00 | 3558 | Ajax vs Benfica | 1.40 | 5.38 | 6.17 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# KIDUKU AJA NA 'HESHIMA KWA MAMA' AKIMVAA KABANGU

**Na Saada Akida**

BONDIA Mtanzania, Twaha Kassim (Twaha Kiduku), amesema amejiandaa vizuri kumheshimisha mwanamke katika pambano lake la Machi 26, mwaka huu, dhidi ya Alex Kabungu raia wa DR Congo mwenye makazi yake nchini Afrika Kusini.

**Pambano hilo la kuwania mkanda wa ubingwa wa UBO katika uzito wa Super Middle litafanyika mkoani Morogoro katika Ukumbi wa Tanzanite ambao upo karibu kabisa na Kituo Kikuu cha Mabasi ya mikoani, Msamvu.**

Bondia huyo ambaye atashuka ulingoni akiongozwa na kaulimbiu ya "Heshima kwa Mama" ikiwa ni lengo kubwa la kuipa heshima inayostahili kwa mwanamke.


Katika pambano hilo, bondia nguli, Abdallah Pazi (Dulla Mbabe) atakuwa miongoni wa wageni waalikwa kushuhudia Kiduku akizichapa dhidi ya Kabangu. Akizungumza na gazeti hili jana, Kiduku alisema imepita miaka minne bila ya yeye kushiriki katika pambano lolote akiwa Morogoro zaidi ya Dar es Salaam.

Alisema mara nyingi kwa miaka hiyo alicheza mapambano yake Dar es Salaam, hivyo sasa anataka kuwapa burudani watu wa Morogoro kwa pambano hilo kupigwa mkoani humo.

"Najua mashabiki wangu mtaku-wa 'mmenimisi' kuniona ulingoni ndani ya Morogoro yetu kwa sababu ni muda sasa sijacheza hapa na ilikuwa ahadi yangu kwamba mwaka huu nipiganie hapa Morogoro," alisema na kuongeza:

"Binafsi maandalizi yanaenda vizuri, mashabiki wasiwe na shaka, nimejipanga vizuri na kikubwa ni mjitokeza kwa wingi siku ya pambano kushuhudia ninavyompiga Kabangu," alisema Kiduku.

Alisema ana matarajio makubwa watu wa Morogoro watamuunga mkono kijana wao na kwamba atahakikisha hatowaangusha na atapigania mkoa wake pamoja na taifa kwa ujumla.



# Kocha Mbeya City atoa sababu kipigo



**Na Adam Fungamwago**

BAADA ya Mbeya City kupoteza mechi yake ya kwanza ikiwa uwanja wake wa nyumbani wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya kwa kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar Jumamosi iliyopita kwenye mechi ya raundi ya 18 ya Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mganda Mathias Lule (pichani), ametaja "kiwango" kama moja ya sababu ya kupoteza.

Matokeo hayo yanaifanya timu ya Kagera Sugar kuwa ya kwanza kuifumua Mbeya City kwenye uwanja wake wa nyumbani, kwani ilikuwa na rekodi nzuri ikicheza hapo mzunguko wa kwanza bila kupoteza.

Lilikuwa ni bao la dakika ya 20 lililofungwa na straika tegemeo wa Kagera Sugar, Hassan Mwaterema lililozima ndoto ya Mbeya City ya kucheza msimu mzima bila kupoteza ikicheza Uwanja wa Sokoine.

Hata hivyo kocha wa timu hiyo, Lule, alikiri kuwa kwa siku za karibuni timu yake haipo kwenye kiwango chao cha kawaida na kwamba kimeshuka kwa sasa na si kama kile walichokuwa nacho mwanzo wa msimu.

"Tumeshuka, siku hizi hatupo kwenye kiwango kizuri, mfano mechi hii wachezaji wangu mwanzoni hawakucheza kwa kufuata maelekezo niliyowapa, walikuja kubadilika mwishoni wakati muda umeshapita. Lakini pamoja na yote tutarudi mazoezini kuangalia namna ambavyo tunaweza kurudi kwenye kiwango chetu kilichozoeleka," alisema Mganda huyo.

Naye Kocha Kuu na Kagera Sugar aliwasifu wachezaji wake akidai sasa wameanza kuingia kwenye mfumo wake anaoutaka.

"Mechi ilikuwa ngumu, ila wachezaji wangu wameanza kuingiza vitu kwenye mfumo wangu. Lakini bado kidogo kwa sababu sisi tuna rekodi nzuri sana ugenini, pia hatuna rekodi nzuri tukicheza Kaitaba," alisema.

Michezo
Jumanne Machi 15, 2022
Nipashe



Tuchel: Sina mpango na Man Utd UKURASA 21

# Ibenge aitabiria Simba fainali CAF

## Pablo aguna, asema ngoma bado ngumu Kundi D, aelekeza...

**Na Saada Akida**

LICHA ya Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, kukiri bado kuna kazi ngumu ya kufuzu hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika hasa katika Kundi lao la D, kutokana na kuwapo kwa ushindani mkubwa, Kocha wa RS Berkane ya Morocco, Florent Ibenge, anawaona 'Wekundu wa Msimbazi' hao wakicheza fainali ya michuano hiyo msimu huu.

**Ibenge juzi alishuhudia kikosi chake, kikikubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Simba kwenye mechi ya Kundi D, iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, matokeo yaliwafanya Wekundu wa Msimbazi hao kukaa kilele ni kwa pointi saba wakifuatiwa na Asec Mimosas wenye alama sita sawa RS Berkane huku US Gandamarie ikiburuza mkia na pointi zake nne.**

Akizungumza na mwandishi wetu baada ya mchezo huo ambao Simba ilimiliki mwanzo mwisho, Ibenge ambaye hajawahi kupata ushindi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Simba tangu akiinoa AS Vita ya DR Congo, alisema Wekundu wa Msimbazi hao wamekuwa katika kiwango bora kwa misimu minne mfululizo waliyocheza Ligi ya Mabingwa Afrika na sasa Kombe la Shirikisho.

Alisema hilo limewasaidia kujenga kikosi imara kinachoweza kupambana popote pale barani Afrika na kupata matokeo mazuri, jambo ambalo hatashangaa kuiona ikifika fainali ya Kombe la Shirikisho msimu huu.

"Kwa misimu minne Simba wamepata wakati mzuri kucheza michezo migumu kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, hilo limewajenga vizuri, kwa hiyo kucheza Kombe la Shirikisho msimu huu, naamini wanaweza kufika fainali na hata kutwaa ubingwa.

"Lakini Simba inaonekana imejiandaa vizuri, na wanaonekana kuwa na kikosi imara na chenye malengo makubwa, jambo ambalo nilitarajia upinzani tofauti," alisema Ibenge ambaye Jumapili ijayo watakuwa ugenini nchini Niger kuivaa US Gandamarie kabla ya kurejea nyumbani kuhitimisha hatua ya makundi dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast.

Kuhusu kushindwa kupata matokeo dhidi ya Simba katika Uwanja wa Mkapa tangu akiwa na AS Vita, Ibenge, alisema: " Sababu kubwa ni kutokana na ukubwa wa Simba, ni timu bora yenye wachezaji wazuri wenye uwezo mkubwa ndio maana nimekuwa nikikumbana na ugumu dhidi yao".

Hata hivyo, wakati Ibenge akiyasema hayo, Kocha wa Simba, Pablo, alisema amefurahishwa na kiwango walichokionyesha juzi, lakini bado wana kazi ngumu kuweza kutinga robo fainali.

Pablo alisema wachezaji wake walijitoa kuhakikisha wanabaki na alama tatu licha ya kwamba malengo yao yalikuwa kupata ushindi mnono zaidi, lakini mambo yalienda tofauti kutokana na presha kubwa waliyokuwa nayo.

"Ulikuwa mchezo mgumu wapinzani wetu walikuwa bora, tulitengeneza nafasi nyingi za kufunga, lakini hatukuwa vizuri katika eneo la umaliziaji tunarudi kujipanga kwa ajili ya mchezo ujao," alisema Pablo.

Alisema baada ya mchezo huo sasa wanajipanga kufanya maandalizi ya kutosha kwa ajili ya mechi ijayo dhidi ya Asec Mimosas ugenini ili kujiweka katika mazingira mazuri katika kundi hilo.

"Baada ya mchezo huu tunatakiwa kusonga mbele na kuwa makini katika michezo miwili iliyobaki kwenye kundi hili, tunaenda kutafuta pointi muhimu ugenini na baadaye kurejea nyumbani kutafuta ushindi," alisema Pablo ambaye kikosi chake kitamalizia hatua ya makundi nyumbani, Uwanja wa Mkapa dhidi ya US Gandamarie.

HUAMINI?...



Winga wa RS Berkane, Tuisila Kisinda (kushoto), akishindwa kuamini na kuishia kushangaa namna Kiungo wa Simba, Pape Sakho, anavyoshangilia baada ya nyota huyo raia wa Senegal kuifungia timu yake bao pekee wakiibuka na ushindi wa 1-0 kwenye mechi ya Kundi D ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **PICHA: SIMBA**

## Mayele apewa ng'ombe wake

**Na Shufaa Lyimo**

HATIMAYE shabiki wa Klabu ya Yanga, Mauya Kanduru, ambaye aliahidi kumzawadia ng'ombe mshambuliaji wa timu hiyo, Fiston Mayele, amekabidhi rasmi zawadi hiyo sambamba na mbuzi mmoja maalum kwa ajili ya kutoa pole kwa Bosi wa Kampuni ya GSM inayoidhamini klabu hiyo, Ghalib Said Mohamed, aliyefiwa na baba yake mzazi hivi karibuni.

Kanduru aliahidi kumzawadia Mayele ng'ombe mwenye thamani ya Sh. 550,000 baada ya kuelezea kuvutiwa na kiwango chake wakati akiiongoza Yanga kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Februari 23, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati akimkabidhi ng'ombe huyo, Kanduru alisema atakuwa anaendelea kutoa zawadi kwa Mayele kila anapotetema (anapofunga).

"Zawadi hii nilimwahidi Mayele tukiwa Morogoro, tumefika jana usiku nikiwa nimeambatana na mke wangu, lakini si ng'ombe tu na mbuzi mmoja kwa ajili ya kumpa pole Mdhamini wa Yanga, GSM," alisema huku akiahidi kuendelea kushirikiana na klabu hiyo.

Kwa upande wa Mayele: "Nimefurahi kuona zawadi hii ambayo nimepewa na shabiki wa Yanga, nimeamini kuwa Wanayanga wanaipenda klabu yao".

Alisema kwao kama wachezaji alichokifanya mwanachama huyo kitawapa morali ya kuendeleza ushindani.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli alisema baada ya makabidhiano hayo watamsajili yeye na mkewe kuwa mwanachama wa Yanga Tawi la Kariakoo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >